# Haribu Kwa Kugusagusa Muhtasari Wa Kitabu Cha Mormoni

Kiswahili Edition

Kimeandikwa Na;

Brian E. McIndoo
Na
Marlene Oar

Kielezo na

Donald E. McIndoo

*MLANGO WA KWANZA*

# KITABU CHA MORMONI NI NINI?

Kitabu cha Mormoni ni habari ya uhamiaji wa kale uliochana mara tatu; jamii ya watu waliongozwa na Mungu kutoka ulimwengu wa zamani hadi America. Kinatwambia vile Mungu aliwaokoa kutoka kwa mikono ya maadui zao na kuwapa nchi ya ahadi. Ni historia ya wafalme, dhini, vita na kuinuka na kuanguka kwa mataifa makuu.

**Wa kawanza** wa hii uhamiaji tatu walikuwa watu waliotajwa kama wayaredi. Mtu kwa jina Yaredi na ndugu yake mwaminifu, aliyetajwa kama ndugu wa Yaredi, waliongoza huu uhamiaji. Yaredi na ndugu yake pamoja na jamaa zao na jamaa wa marafiki wachache waliacha mnara mkuu wa Babeli. Katika wakati Mungu alichanganya lugha, tukia mwaka 2200 kabla kristo kuzaliwa. (Mwanzo 11:5-9 na Etheri 1:7-9).

Walipita nchi mpaka walifika kwenye bahari. Waliunda mashua kubwa nane na kutwika kuenda mbele baharini, wakiendeshwa juu ya maji na upepo na mikondo. Baada ya siku mia tatu na arobaini na nne walifika kwa ukingo wa nchi ya ahadi ambaye Bwana mwenyewe aliwandalia. Hii nchi ya ahadi ilitokea na amri za milele. Wale ambao watamiliki nchi ni lazima wamtumikie yule Mungu wan chi, ambaye ni Yesu Kristo, au waondolewe wote na waangamizwe. (Etheri 1:29-35).

Taifa kuu la Yaredi walikosa kutii onyo na waligeuka kutoka kwa Mungu. Mfalme koriantumuri alikataa kusikia mashauri na mwito wa kutubu kutoka kwa nabii Etheri. Hivyo taifa la Yaredi liliangamizwa katika vita via wao kwa wao isipokuwa kwa mtu mmoja, koriantumuri. (Etheri 6:72-73).

**Uhamiaji wa pili** wa watu wanajulikana kama WaNefi. Lehi alikuwa kutoka jamaa ya Yusufu, yule yule Yusufu ambaye alikuwa kijana wa Yakobo na aliuzwa katika misiri na ndugu zake kwamba aweze kulinda baba yake, Yakobo, na watu wa nyumbani mwake kutoka kwa kutaabishwa pamoja na njaa. Kwa sababu Lehi alikuwa ametangaza kwa uaminifu hadi kwa wenyeji wa Yerusalemu uharibifu wa karibu sana wa Yerusalemu na kushuhudia uovu wa watu, na kuja kwa Mesiah, kulikuwa na mapatano ya shauri la kumuua. Katika ndoto, Lehi alishauriwa kuchukua jamii yake na kukimbia nje ya Yerusalemu. Lehi alichukua mke wake Sariah na vijana wake wane, Lamani, Lemueli, Samu na Nefi, pamoja na Ishimaeli na jamaa yake walivyo kuwa wakitoka Yerusalemu. Walianza safari yao wakati wa mwaka wa kwanza wa utawala wa Zedekia, mfalme wa Yuda. Historia inatuambia utawala wa Zedekia ulianza katika mwaka 596 kabla Kristo kuja. (Mwanzo 49:22; 1Nefi 2:7, 8 na 1Nefi 1:3, 18-20; 164, 165).

Kwa mwujiza, Mungu aliongoza Lehi na jamaa yake kupitia nyikani, kisha kupitia bahari mpaka nchi ya ahadi. WaNefi walichukua kumbukumbu ya watu wao kuhifadhi lugha ya Baba zao, maneno ya manabii na historia ya watu wao. (1Nefi 1:26, 54; 1Nefi 5:176-178: 1Nefi 5:78-72 na 1Nefi 1:82, 83, 159).

Mugawanyiko ulitokea kati ya Nefi na Ndugu zake, ukileta laana juu ya Lamani, jamaa yake na wale ambao walimfuata na wakapata kuitwa kama Walamani. Zilianza vita kuu na ugomvi kati ya WaNefi na Walamani. Wakati wote, WaNefi pia wakapata kuwa waovu kama Walamani. Katika mapigano makuu katika nchi ya Kumora Mungu aliwafanya WaNefi waweze kuangamizwa kwa sababu walikuwa wamegeuka kutoka kwake kwenda kwa uovu. (1Nefi 3:128-134; 2Nefi 4:27-41; Omni 1:14; 4Nefi 1:44-53 na Mormoni 2:12-14; Mormoni 2:1, 3; Mormoni 3:3, 10-13 na Mormoni 4:1, 2, 6-9).

**Kuhama watatu** unaitwa kama wamuleki. Wamuleki pia walitokea wazi Yerusalemu wakati wa utawala wa mfalme Zedekia. Walianza uhamiaji wao miaka michache baada ya WaNefi kwa wakati mfalme Zedekia alichukuliwa katika mateka kuenda Babeli, mwaka 587 kabla kristo. Muleki alikuwa kutoka kabila ya Yuda na mmoja wa vijana wa mfalme Zedekia. Muleki alikuwa mdogo dhahiri kutamburika kuitwa mtoto na alipona kuwawa pamoja na ndugu zake wakati Yerusalemu uliangamizwa. (Yeremia 39:1-2; 6-7).

Muleki na baadhi ya jamaa yake pia waliongozwa na Bwana kwa nchi ya ahadi na walikaa katika eneo inayoitwa nchi ya Zarahemia. Watu wa Zarahemia, (Wamuleki), waligunduliwa na WaNefi katika nchi ya Zarahemia. Wamuleki waliungana wao kuingia taifa la waNefi. (Helamani 3:55-57; 2:129; Omni 1:23-26)

# *MLANGO WA PILI*

# NI JINSI GANI KITABU CHA MORMONI KILITOKEA?

Kijana wa Lehi, Nefi alitunza kumbukumbu iliyoandikwa kwa kuyaandika juu ya pamba ya mfua chuma. Namna moja iliitwa pamba za Lehi na ilikuwa na ndoto nyingi na maono, unabii na nasaba. (1Nefi 2:1-3, 92).

Maandiko ya Nefi, bamba kubwa ya Nefi, ilichukua ndani muhtasari wa Bamba za Nefi, hesabu kamili ya historia ya WaNefi, utawala wa wafalme, vita na ugomvi na kuonekana kwa Yesu kristo. Kumbukumbu hii ilianza na Nefi lakini ilipokelezwa kutoka kizazi hadi kizazi, kila mwandishi akiendeleza kazi ya kuhifadhi Historia. (1Nefi 5:219, 1Nefi 1:17, 1Nefi 3:1; 1Nefi 2:93-97; 1Nefi 5:218, 222 na 2Nefi, 3:27)


Kikundi kingine za Bamba, Bamba ndogo, pia inatajwa kama bamba za Yakobo, zilihifadhiwa kwa kusudi maalum kwa Mungu. Zilikuwa na hesabu ya maisha na kazi ya Nefi, na unabii na maagizo kutoka kwa Mungu. Hii tena ilipitishwa kutoka kizazi hadi kizazi mpaka miaka mia tatu na ishirini baaba ya kristo wakati Ammoroni alificha maandiko katika kilima kilichoitwa shemu; (1Nefi 2:92-99; 2Nefi 3:28; Yakobo 2:69 na Yoramu 1:2, 4Nefi 1:57-59).

Ammoroni aliagiza kijana wa miaka kumi aliyeitwa Mormoni, wakati atafika umri wa miaka ishirini na nne aende na kupata tena Bamba za Nefi kutoka shimu, aache Bamba zingine katika ardhi.  Pia alimuagiza Mormoni kuchora juu yake vitu vyote amevyiona juu ya watu wa Nefi.  Miaka kumi na nne baabaye, Mormoni alikumbuka maneno ya Ammoroni na alifuata maagizo yake na kuongeza maneno yake, yaliyoitwa kama maneno ya Mormoni kwa Bamba za Nefi.  (Mormoni 1:1-6 na maneno ya Mormoni 1:13-15).

Kabla ya maangamizi ya utamaduni ya WaNefi, Mormoni alirudi kwa kilima shimu na kuchukua maandiko yote Bwana alikuwa amekabidhi kwake ili yazianguke katika mikono ya maadui zao, Walamani. (Mormoni 2:25).

Mormoni alifupisha maandiko, akiongeza maneno machache yake mwenyewe kabla yakuyaficha yote katika kilima kumora, isipokuwa kwa ufupisho, ambao alikabidhi kijana wake Moroni ambaye alimaliza hesabu ya utamaduni ya WaNefi (Mormoni 3:3-8, 4:1-6).

Moroni, WaNefi wa mwisho alikuwa anazidi kuishi, alichukua ufupisho wa maandiko aliyepewa na Baba yake Mormoni na kuongeza maneno yake mwenyewe na mafunzo ya Baba yake.  Moroni pia aliongeza kwa ufupisho wa Baba yake hesabu toka Bamba za dhahabu ishirini na nne, zilizoitwa kama kitabu cha Etheri. (Etheri 1:1-6).



Etheri, Myaredi nabii, alijificha katika pango alipokuwa akitazama maangamizi ya Wayaredi wao kwa wao katika vita vikuu.  Etheri aliandika historia yao, na hapo akificha maandiko yake hadi watu wa Limhi watakapo ya vumbua.  Mfalme wa WaNefi, Mosia, ambaye alikuwa na karama ya ufahamu, alitafusiri maandiko. (Mosia 5:62-79; 9:170; 12:14, 22).

Tukia mwaka 421 baada ya kristo (A.D.) haya maneno yasiofutika yaliyoandikwa juu ya Bamba za dhahabu yalizikwa katika ardhi na Moroni na yalibaki yamezikwa ardhini kwa miaka kumi na nne, yakingojea kwa siku wakati Mungu atayaleta tena kwa kizazi kijao.

**************************

Mapema mwaka 1800 nakuendelea ilikuwa majira ya ufufuo mkuu katika serikari ya juu New York.  Kijana wa miaka ya kati alipatwa na mzigo katika moyo wake kujua mapenzi ya Mungu.  Kama ni kanisa gani anaweza kujiunga nayo.  Wakati akisoma waraka wa Yakobo katika bibilia yake, alipitia haya maneno ya upuzio; "lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa". Akishawishiwa na fungu la maneno, Yusufu smith alijua ni lazima afanye kama Yakobo aliagiza au abaki katika giza.  Wakati wa masaa ya asubuhi ya siku nzuri wazi mapema mwanzo wa mwaka 1820, Yusufu mdogo alirejea porini, sio mbali kutoka kwao nyumbani Manchester, New York, kuchunguza kwa bwana kama ni dini gani ambaye ilikuwa ya haki.  Akijipata yeye mwenyewe

katika mahali padogo yaliyotulia, alipiga magoti chini na alianza kutoa maombi yake. Yusufu alisimulia habari iliotukia kuwa kama kutwaliwa kwa nguvu Fulani, ambaye ilimshinda kabisa alimwita Mungu kumuokoa. Alipopata kuwa na mshtuko wa hofu kama nini kilikuwa kinaendelea, aliona nguzo ya mwangaza kamili juu ya kichwa chake, ikishuka taratibu mpaka ilipoanguka juu yake. Wakati mwangaza ulipotulia juu yake, Yusufu aliona watu wawili mashuhuri wakisimama juu yake angani. Mmoja wao alizungumza, akimwita Yusufu kwa jina, na kusema *"Huyu ni mwanangu mpendwa msikilize"*.

Yusufu aliuliza mtu mashuhuri ni ipi ya madhehebu yote ilikuwa ya haki, na ambaye ataweza kujiunga. Mtu mashuhuri alimwambia Yusufu asijiunge na yoyote kwa sababu imani yao yote ilikuwa chukizo, na yote yameharibika.

Yusufu Smith alipatwa na mateso mengi kwa mikono ya viongozi wa dini ye yote aliambia kuhusu kukutana kiroho pamoja na watu mashuhuri, walakini alibaki imara katika imani yake kuhusu maono yake. Katika tarehe 21 Septemba mwaka 1823, huku akilala juu ya kitanda chake akiomba, Yusufu alipata maono ya pili. Yusufu alihadithia kama hivi; wakati nilipokuwa katika tendo la kumwiita Mungu, niligundua mwangaza ukitokea chumbani ambao uliendelea kuongezeka mpaka chumba ilikuwa yenye kuwasha kuliko adhuhuri: "Papo hapo mtu mashuhuli alionekana kando ya kitanda changu, akisimama hewani kwa sababu miguu yake haikugusa chini.

"Wakati wa kwanza nilimwangalia niliogopa, lakini mara moja hofu ikaniacha. Aliniita kwa jina, na akaniambia kwamba alikuwa mjumbe aliyetumwa kutoka machoni pa Mungu kwangu, na kwamba jina lake lilikuwa Moroni. Kwamba Mungu alikuwa na kazi kwangu kufanya, na yakwamba jina langu litakuwa kwa mema na mabaya Miogoni mwa mataifa yote, jamaa na lugha; au kwamba litazugumzwa yote vyema na ubaya miongoni mwa watu wote.

Alisema kulikuwa kitabu kiliwekwa, kilioandikwa juu ya bamba za dhahabu, kinatoa hesabu ya zamani ya wenyeji wa bara hili, na asili kutoka wapi walitokea. Alisema pia kwamba injili kamili ya milele ilikuwa ndani yake, kama ilihifadhiwa na mwokozi kwa wenyeji wa kale. Pia ya kwamba kulikuwa na mawe mawili katika upindi za fedha, na haya mawe yamefungwa kwa Bamba iliyofanya kile kinachoitwa urimu na thummimu, iliyowekwa pamoja na bamba na kumiliki na matumizi ya haya mawe ndiye yalitambua hapo kale au wakati wa kwanza, na yakwamba Mungu aliyandaa kwa kusudi la kutafsiri kitabu."[2]

Wakati Yusufu alipokuwa akizungumza pamoja na mtu mashuhuri, tokea lilipofunguliwa katika moyo wake. Aliona ni wapi bamba za kale zilifichwa dhahiri kabisa na kupambanuliwa ya kwamba baadaye ilikuwa rahisi kwa Yusufu kutambua mahali penyewe wakati atakapoyaona. Akivumbua jiwe kubwa, Yusufu aliondoa kwa uangalifu udongo kutoka kando kando yake, akifunua kisanduku cha mawe. Akiondoa kifuniko cha mawe na wenzo, Yusufu aliweza kutazama ndani na kuona urimu na themmimu na sahani ya Bamba. Kusudi la Yusufu ilikuwa ni kuondoa bamba; walakini, malaika alitokea tena na kumwambia kwamba wakatihaujafika bado. Malaika aliagiza Yusufu kurudi sehemu ile ile halisi kwa mwaka moja na kuweza kuendelea kurudi kila mwaka mpaka wakati uliowekwa uje kwake kupata bamba kutoka kisanduku cha mawe kwa kupatana na amri, Yusufu alirudi kila mwaka, kila wakati akimpata

mjumbe yule yule pale na kupata maagizo kutoka kwake. Wakati Yusufu alirudi hadi mahali iliowekwa katika mwezi Septemba mwaka 1827, mjumbe alipeana yaliyomo sanduku ya mawe kwake kama alivyoahidiwa. Ilikuwa ni wajibu wa Yusufu kutunza na kulinda hii vitu hadi mjumbe arudi na kuvikusanya na kutafsiri bamba kwa kutumia urimu na Thummimu.

Kazi ya kutafsiri kitabu cha Mormoni haikuanza hadi Aprili wa mwaka 1829. Yusufu anasimulia vile alianza, "katika siku ya kumi na tano wa Aprili, elifu moja mia nne na ishirini na tisa, Oliver Cowdery, alikuja kwa nyumba yangu hadi siku ile sikukuwa nimemwona. Akaniambia ya kwamba akiwa mwenyewe akifundisha shule ya ujirani mahali baba yangu alikaa; na Baba yangu akiwa mmoja wa wale ambao walitumwa kwa shule; alienda kwa halimashauri ya wakati wa mwaka wa nyumba ya Baba yangu, na akiwa pale familia ilimtolea habari kwake tukio langu kupata bamba; na kwa sababu hiyo alikuwa amekuja kufanya hoja juu yangu"[3.]

Baada ya siku mbili wa mfiko wa Oliver Cowdery (ikiwa siku ya kumi na saba ya aprili), Yusufu alianza kutafsiri na Oliver akiyaandika maneno. Oliver Cowdrey aliandika kuhusu kazi "Hii ilikuwa siku si ya kusahaulika kamwe- kukaa chini ya sauti ya maono yakiamuruliwa na upuzio wa mbinguni, uliamsha shukrani ya juu sana wa hii moyo. Siku baada ya siku niliendelea, bila kuzuiwa, kuandika kutoka kinywa chake alipokuwa akitafusiri pamoja na urimu na Thummimu … historia au kumbukumbu inayoitwa Kitabu cha Mormoni"[4]

Katika mwezi wa sita wa mwaka 1829, utafsiri ulikamilika na haki yote ya kitabu ilibuniwa ya kuzuia wengine wasikifuatishe. "Baada ya Yusufu na wengine walikuwa wamefanya shauri pamoja na weneza habari wengi, E.B. Grandini, mwenyeji na msimamisi wa wayne sentineli, alikubali kupiga chapa kitabu … mkataba ulitiwa sahihi tarahe 25 mwezi wa nane, mwaka 1829, kwa jumla ya nakala za vitabu Elifu Tano."[5] Kwa wakati huu Yusufu Smith pia alirudisha bamba na Urimu na Thummimu kwa mjumbe wa mbinguni ambaye alikuwa amevipeana kwa mikono yake.

# *MLANGO WA TATU*

## KUSUDI LA KITABU CHA MORMONI NI NINI?

Kitabu cha Mormon, kinakusudia kuwa ushuhuda thabiti kwa Bibilia Takatifu kwa njia nyingi. Moja ya sura ya maana nyingi kupita yote ni ya kwamba inatufundisha kuamini injiri ya wokovu katika Yesu Kristo vile imeandikwa katika Bibilia zetu. Kitabu cha Mormoni kinasema; "K*wa hivyo tubuni, na mbatizwe katika jina la Yesu, na mkubali injili ya Kristo, ambayo itawekwa mbele yenu, sio tu kwa maandishi haya, lakini pia kwa maandishi ambayo yatawajia wayunani kutoka kwa wayahudi, maandishi ambayo yatatokea kwa wayunani hadi kwenu. Kwani tazama, haya yameandikwa kwa kusudi kwamba mngeamini hayo; na mkiyaamini hayo mtaamini haya pia; na ikiwa mtaamini haya mtajua kuhusu babu zenu, na pia kazi za*

*ajabu ambazo zimesababishwa na uwezo wa Mungu miongoni mwao." ( Mormoni 3:30-31)* Pia inazungumza juu ya habari imeandikwa katika kitabu cha Mormoni na Bibilia kuwa moja katika kusudi. *"Na maneno ya mwanakondoo yatafumbuliwa katika maandishi ya mbegu yako, vile vile katika maandishi ya wale mitume kumi na wawili wa mwanakondoo. Kwa hivyo zote mbili zitaunganishwa kuwa moja; kwani kuna Mungu mmoja na mchungaji mmoja ulimwenguni kote." (1 Nefi 3:195-197)*

Ahadi nzuri, *"Kwani kuna Mungu mmoja na mchungaji mmoja ulimwenguni kote,"* inatukumbusha Mungu hana upendeleo na watu. Mpango wake wa wokovu na injiri yake ni sawa kwa kila mwanadamu wa kila taifa ya ulimwengu. Wakati Yesu alitembea katika Palestina alisema, *" Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili, na hao nao imenipasa kuwaleta, na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja." (Yohana 10:16)* wengi walifikiri ya kwamba alikuwa akizungumuza juu ya wayunani, walakibi si hivyo. Alieleza kwa wanafunzi ya kwamba, yeye mwenyewe atafundisha kwa nyumba ya Israeli. *"Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Mathayo 15:24).*

Makabila mengine ya Israeli yalitawanyika juu ya nchi nyingi na visiwa via bahari, na baada ya kufufuka kwake, Yesu alitembelea hizi kondoo zingine wa nyumba ya Israeli. Kitabu cha Mormoni kinashuhudia kwa hii hadhi kuwa imetimizwa. " Na kweli na waambia, kwamba ni nyinyi ambao nilisema; kondoo wengine ninao ambao sio wa zizi hili; hao nao ninapaswa kuwaleta, na watasikia sauti yangu; na kutakuwa na kusudi moja, na mchungaji mmoja; na hawakunielewa, kwani walidhani kwamba nilizungumza kuhusu wayunani; kwani hawakuelewa kwamba wayunani watageuka kupitia mahubiri yao; na hawakunielewa kwamba nilisema wataelewa sauti yangu; na hawakunielewa kwamba nilisema wataelewa sauti yangu; na hawakunielewa kwa wayunani hawatasikia sauti yangu wakati wowote kwamba sitajidhihirisha kwao isipokuwa kupitia kwa Roho matakatifu. Lakini tazama, nyote mmesikia sauti yangu, na kuniona; na nyinyi ni kondoo wangu, na mmehesabiwa miongoni mwa wale ambao Baba amenipatia; na kweli, kweli nawaambia ninao kondoo wengine, ambao si wanchi hii, wala ya Yerusalemu, wala mahali popote katika chi ya karibu niliyotoa huduma; kwani wale ambao ninawazungumzia ni wale ambao bado hawajasikia sauti yangu; wala sijajidhihirisha kwao; lakini nimepokea amri kutoka kwa Baba kwamba niwaendee, na kwamba watasikia sauti yangu, na watahesabiwa miongoni mwa kondoo wangu; ili kuwa na kundi moja na mchungaji mmoja; kwa hivyo nitajidhihirisha kwao." 3 Nefi 7:20-26.

**********************

Mtume Paulo aliwambia wagalatia, "mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe." Kitabu cha Mormoni kinashuhudia hiyo wazo na kinafundisha injili sawa kama Bibilia. Kinafundisha injili sawa ya wokovu, ambaye ni lazima uamini katika Kristo, ni lazima utubu, ni lazima upate kuwa kama mtoto mdogo, lazima ubatizwe, ni lazima uwe mtiifu na ni lazima uvumilie hadi mwisho.

Kitabu cha Mormoni kinafundisha maagizo sawa ya injili ndani katika Bibilia, ambayo ni; kubarikiwa kwa watoto wadogo, uponyaji wa wagonjwa kwa kuekea mikono; upokeaji wa Roho mtakatifu, ubatizo kwa kutumbukiza majini, kufanya kasisi kwa kutiwa mikono na hitaji ya kutwaa meza ya Bwana.

Kitabu cha Mormoni kinatufundisha kufuata utaratibu sawa wa kanisa vile Kristo aliiweka imara katika Bibilia. Kanisa ilianzishwa juu ya Kristo, mwamba, kanisa iliitwa baada ya Kristo, imani iwekwe juu ya msingi wa Mungu asiobadilika, Kristo aliita kumi na wawili kuwa wajumbe wa kanisa katika ulimwengu na kanisa ina dumishwa kwa karama za roho mtakatifu.

Akutakuwa na injili mpya ya wokovu itakapotokea, walakini Mungu aliweza kutuambia atatupa mambo yake na maagizo kutoka mara kwa mara. *“ Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo. (Isaya 28:10).*

Kitabu cha Mormoni kinatimiza unabii mwingi na ahadi ndani ya Bibilia. Ahadi ya kwanza ni kubarikiwa kwa Yusufu na baba yake, Israel ambaye alisema nchi ya Yusufu itabalikiwa. Tunasoma; “na Yusufu akanena, nchi yake na ibarikiwe na Bwana, kwa vitu vya thamani vya mbinguni, kwa huo umande, na kwa kilindi kilalacho chini, na kwa vitu vilivyo bora vya matunda ya jua, na kwa vitu vilivyo bora vya maongeo ya miezi, na kwa vitu viteule vya milima ya kale, na kwa vitu vilivyo bora vya vilima vya milele, kumbukumbu la *Torati 33:13-16*.

Bibilia pia inatwambia ya kwamba nchi ya Yusufu itakuwa ngambo ya Bahari. *“Yusufu ni mti mchanga mwenye kuzaa, mti mchanga wenye kuzaa karibu na chemichemi, matawi yake yametanda ukutani”, Mwanzo 49:22.* Kwa maneno ya manabii, tunajifunza ya kwamba kwa unabii ukuta inatoa mfano wa Bahari. *“ Je! wewe u mwema kuliko Noamoni, uliowekwa kati ya mito, uliozungukwa na maji; ambao boma lake lilikuwa bahari, na bahari ilikuwa ukuta wake?” (Nahumu 3:8).*

Ahadhi nyingine ni kutakuwa na vitabu viwili katika mikono yetu, kimoja kwa Yuda, ambaye tunajua kama Bibilia and kingine kwa Yusufu na wazao wake, ambaye ni kitabu cha Mormoni. Vitabu hivyo viwili vinatumika pamoja kama kimoja, kwa maana vinachukua ndani utimilifu wa injili. *“Na wewe mwanadamu, twaa kijiti kimoja; ukaandike juu yake, kwa Yuda, na kwa wana wa Israeli wenzake; kisha, twa kijiti cha pili; ukaandike juu yake, kwa Yusufu, kijiti cha Efraimu, na kwa nyumba yote ya Israeli wenzake; ukaviunge pamoja kwa ajili yako hiki na hiki viwe kijiti kimoja, viwe kimoja katika mkono wako.” (Ezekieli 37:16-20)*

Bibilia inataja hii kitabu cha Yusufu, ambaye kitatokea mbeleni, kazi ya kushangaza na ajabu, kwa sababu wale ambao wamekuwa vipovu kiroho na mafundisho ya dini ya mwanadamu wataona ukweli mara ya pili. *“Na maono yote yamekuwa kwenu kama maneno ya chuo kilichotiwa muhuri, ambacho watu humpa mtu aliye na maarifa, wakisema, tafadhali ukisome hiki; akisema, siwezi, kwa kuwa kimetiwa muhuri; na katika siku hiyo viziwi watasikia maneno ya hicho chuo, na macho ya vipofu yataona katika upofu na katika giza. Wanyenyekevu nao wataongeza furaha yao katika Bwana, na maskini katika mwanadamu watafurahi katika mtakatifu wa Israeli.” (Isaya 29:11, 18, 19).*

Haikukuwa kazi rahisi kwa mwanadamu kutunza maandiko ya zamani kwa kuyaandika juu ya Bamba ya chuma. Bidii nyingi ilikuwa ifanyike kutafuta na kukusanya mawe yenye madini moja, yeyusha na kuifanyiza kuwa Bamba nyembamba ya chuma, halafu anaandika juu yao. Hata hivyo, Mungu aliamuru watu kuaandika na kuipitisha habari kwa wengine kuandika kwa kusudi maalumu kwake. Watu waaminifu waliaandika vitu vyote waliona na kusikia kuhusu historia yao, na Mungu akitenda katika maisha yao.

Ikichukuliwa ndani katika ukurasa wa kitabu cha Mormoni tunaweza kugundua nyingi ya hayo makusudi muhimu Mungu alikuwa naye. Ndani ya ukurasa wa kitabu cha Mormoni, Mungu anafumbua hizi makusudi maalumu, kama; maagizo ya watu wake, *1Nefi 5;224-225*; hivyo wote waje kufahamu ya kwamba Yesu kristo ni mwana wa Mungu, *(1Nefi 3;192-194);* kinatumika pamoja na Bibilia kuangamiza mafundisho ya dini ya uongo, kutoa ushindani na kuweka amani *(2Nefi 2:19-21);* kitaleta watu kwa maarifa ya Baba zao na maagano Mungu alifanya pamoja nao *(2Nefi 2:23);* na kama Bibilia takatifu, kuonyesha nguvu zake hadi kizazi kijacho. *(Alma 17:45).*

Mwishowe kitabu cha Mormoni kinakuwa jaribio la Imani. Kwa maneno ya mwisho ya Moroni anafanya maombi kwa kizazi kijacho ambao watapokea hii habari; *"Na mtakapopokea vitu hivi, ningewashauri ya kwamba mngemujulisha Mungu, baba wa milele, katika jina la Kristo, ikiwa vitu hivi si vya kweli' na ikiwa matauliza na moyo wa kweli, na kusudi halisi, mkiwa na imani katika Kristo, atawaonyesha ukweli wake kwenu, kwa uwezo wa Roho mtakatifu. Na kwa uwezo wa Roho mtakatifu mtajua ukweli wa vitu vyote"; (Moroni 10; 4, 5).*

# *MLANGO WA NNE*

## NI KUTOKA WAPI KITABU CHA MORMONI KILIPATA JINA LAKE?

Mormoni ni jina la mtu ambaye alikuwa mwenye kutiwa kazi ya kuchukua maandiko yaliyokuwa ndani juu ya Bamba za chuma ambaye yalikuwa yamepokelewa kutoka kizazi hadi kizazi na kuongeza vitu vyote ambaye alikuwa amevichunguza kuhusu watu wake kwa Bamba za Nefi. Mormoni vile vile alibuni fupisho ya habari zilizoandikwa, ambaye alimpa kwa kijana wake Moroni. Moroni aliandika maneno ya mwisho na alificha ufupisho wa maandiko kwa kusudi yasihalibiwe na iweze kutokea kwa wayunani katika wakati unastahili na kuchukuliwa kurudi kwa nyumba ya Israeli.

Yusufu Smith, ambaye alitafsiri kitabu cha Mormoni kutoka kwa lugha ya kale, yalioamriwa ndani ya maandiko yake, Historia ya kanisa. "Ninapenda kutaja hapa ya kwamba anwani ya ukurasa ya kitabu cha Mormoni ni utafsiri hasa, uliopatikana kutoka ukurasa halisi ya mwisho, kwa mkono wa kushoto wa mkusanyo wa vitabu vya Bamba"[6] antuthibitishia katika maelezo yake ya kwamba anwani, KITABU CHA MORMONI, ni utafsiri harisi hivyo ilioandikwa katika Bamba alitafsiri.

# *MLANGO WA TANO*

# HADITHI ZA WANEFI NA WALAMANI

## LEHI, NABII WA YERUSALEMU

***Lehi Akiondoka Yerusalemu***
(1 Nefi 1:3-6, 10-12, 18-33)

Lehi alikuwa mtu mwaminifu ambaye aliishi katika yerusalemu mwanzoni mwa mwaka wa kwanza wa utawala wa mfalme Zedekia, mfalme wa Yuda, kama mwaka wa 597 ( kabla ya kuzaliwa kwa Yesu). Wakati wa mwaka huo manabiii wengi walitokea Yerusalemu, wakiwambia watu ni lazima watubu, ama mji mkuu Yerusalemu ni lazima uangamizwe.

Siku moja kama vile Lehi alikuwa akiomba nguzo ya moto ilikuja chini kutoka mbinguni na ikatua juu ya mwamba mbele yake. Maono yalitokea mbele ya macho yake juu ya yale yanoyoenda kutokea huku Yerusalemu. Baada ya kupata haya, Lehi alichoka sana, kwa hivyo alirejea nyumbani kupumzika. Lehi akiwa amelala huku akipumzika, Yesu Kristo mwana wa Mungu alijitiirisha mbele yake. Yesu alifungua kitabu na kusema, someni hii. Lehi apoanza kusoma alisikia huzuni kuu alivyoona maovu na vitu vyote vile watu wa Yerusalemu walikuwa wakifanya.

Yesu alifichua kwa Lehi yakwamba kama watu wa Yerusalemu hawatatubu, madui zao watashambulia mji. Madui watakapokuja watawaua watu wengi na kuteka wenti wao na kuwachukua inchi nyingine mbali. Mungu alimwagiza Lehi kuwaonya watu watubu na kama watakataa basi Mungu ataingamiza Yerusalemu.

Watu waovu wa Yerusalemu hawakuamini unabii wa Lehi. Mara ya kwanza walimdhihaki na kudai yakwamba hakuna kitu kitaweza kuangamiza mji waqo mkuu. Walikana kuona maovu yao na hawakuweza kutubu. Mara moja walichoka kusikia mwito wa Lehi wa kutubu, kwa hivyo walishauriana kumua.

Mungu alikuwa na mpango mingine kwa Lehi na familia yake na aliwaonya yakwamba ni lazima wakusanye kwa haraka mali na vitu vyao na waelekee Yerusalemu kwa sababu adui zake walitaka kumuua. Lehi aliagizwa kukimbia mpaka nyikani. Lehi hakujua nini kitatukia kwa jamii yake lakini alimtumainia Mungu.

Ingawa Lehi alikuwa mtu tajiri na alimiliki vitu vizuri vingi, yeye, mke wake Saria na vijana wao walifunga pamoja vile pekee walihitaji kuishi na kuacha kwao na mali yao yote na kusafiri mpaka nyika waishi ndani ya hema. Lehi alimwamini Mungu atalinda jamii yake.

***Bamba Ya Shaba***

Baada ya kusafiri siku tatu, Lehi na jamii yake walifika kambi kando ya mto. Wakati huu wote, Lamani na Lemueli, vijana wakubwa wa Lehi walinungunika, kwa nini tuliacha makao yetu mazuri? Hakuna kutu kitaweza kuharibu mji mkuu Yerusalemu. Baba yetu anawazia jambo lisiloelekea kuwa kweli.

Vijana wa Lehi, Sam na Nefi, waliamini baba yao. Nefi kijana mdogo, alitaka kuelewa maono ya baba kwa hivyo aliuliza Mungu kumuambia kama maono ya baba ni ya kweli.

Hapo Bwana alamsungumzia Nefi, umebarikiwa kwa sababu umeomba na nguvu kujua ukweli. Kama utashika amri zangu nitaongoza jamii yako mpaka nchi mpya. Nefi aliends ndani ya hema ya baba yake kumuambia juu ya yale yaliompata, lakini Lehi alisema Mungu alimzungumzia tena katika ndoto. Alimwagiza Nefi ya kwamba yeye na ndugu zake lazima warudi Yerusalemu kwa nyumba ya Labani. Hapo walikuwa waombe Labani mandiko matakatifu yalioandikwa juu bamba za shaba ambaye ndani yake kuna maandiko ya wayahudi na kizazi cha baba zao. Mungu aliwagiza wao kuchukua haya mandiko mpaka nyikani nao.

Lamani na Lemueli walikataa, wakisema yakwamba ilikuwa hatari kubwa na hawatakikani kwenda. Walakini, Nefi alikuwa na moyo tofauti na aliwasihi sana ndugu zake kusikia maagizo ya Mungu. Kama Mungu akituambia kufanya jambo furani atatupa njia ya kulifanya.

Wakifuata Nefi, hawa wandugu warirudi kwenye mji wa Yerusalemu mahari watu waliongojea kuwaua.

## *Nyumba Ya Laban*

(1Nefi 1:68-95)

Kwa mpaka wa mji wandugu walipiga kura kuamua ni kina nani wao ataenda kwa nyumba ya Labani na kumuuliza hizo Bamba za shaba. Wakati waliopiga kura, Lamani ndiye mmoja alichaguliwa kwenda kwa Labani kumuliza hizo Bamba.

Kwa hofu, Lamani alikwenda kwa nyumba ya Labani na kuuliza kuhusu Bamba za shaba. Labani alihuzunika (alikasirika), akiwashtiki wao kujaribu kumuibia, na kuwamuru watoke. Labani, Lemueli na hata Samu walitia mashaka kwa kutofaulu.

Walikuwa karibu kurudi kwa Baba yao bila maandiko matakatifu, lakini Nefi alisema, wandugu zangu, Mungu anatamani ya kwamba tuwe na neon lake tulichukue pamoja nasi katika safari yetu. Kama Mungu alituamrisha kwenda na kupata Bamba za shaba, kwa hiyo yeye atatayarisha njia kwetu kuitimiza hiyo.

Wandugu hao waliamua kurudi kwao huko Yerusalemu na wapate hazina zao waliacha nyuma wakati walikimbia mji. Labani alikuwa mtu mwenye choyo (tamaa) na walifikiria huenda yeye atawauzia izo Bamba za shaba. Wakati huu wandugu wote walienda kwa nyumba ya Laban wakiwa na dhahabu zao, fedha na mawe ya thamani.

Wakati Labani alipowaona wakija, alliwamuru watumishi wake waende wakawauwe na kuleta hazina yao. Wakati Nefi na ndugu zake waliangalia upande wa nyumba ya Labani na kuona watu wakikimbia upande wao wakitikisa upanga wao juu ya hewa waliogopa. Waliangusha hazina zao na

kukimbia. Wakati walifika mahali pasipo hatari, Lamani, Lemueli walighadhabika sana na kumlaumu Nefi kw kupoteza hazina zao zote na karibu sana kuwaletea kifo. Katika hasira hayo, Lamani na Lemueli, walianza kumpiga Nefi na Samu. Kwa ghafula Malaika akatokea mbele yao na kusema; kwa nini mnampiga ndugu yenu mdogo? Mungu amemchagua Nefi kuwatawala ninyi kwa sababu ya maovu yenu. Rudi Yerusalem na Mungu atamkabidhi Laban kwa mikono yenu.

### *Mungu Akitayarisha Njia*

(1 Nefi 1:104 - 146, 155 - 166)

Usiku ulikuwa umetukia kwa wakati wandugu waliporudi huko Yerusalem kwa hivyo walijificah inje ya ukuta wa mji. Mungu alimwambia Nefi kuenda mpaka nyumba ya Labani. Pole pole, kwa uangalifu, ili kwamba mtu yeyote asimwone. Nefi alitembea kuelekea kwake Labani. Nefi alikuwa peke yake na hakujua ni nini kitaenda kutendeka, alijua pekee ya kwamba Mungu atamtunza.

Wakati Nefi alipofika kwake Laban, alikuta Labani akilala kwa ardhi, mlevi. Mungu alisema; ni lazima umue yeye. Ni vizuri mtu mmoja muovu kufa, kuliko kwa taifa inzima kusahau juu ya Mungu.

Pamoja na dhiki kuu, Nefi alimtii Mungu na alichukua upanga wa Labani na kukata kichwa chake. Akifaa nguo za Labani, Nefi alitembea kwa upande wa hazina mahali Labani alihifadhi hayo maandiko matakatifu akigeuza sauti yake, Nefi aliamuru mtumishi wa Labani afungue mlango kwelekea nyumba ya hazina na kumsaidia kupata hiyo Bamba za shamba. Akiamini ya kwamba Nefi alikuwa Labani. Yule mtumishi alimsaidia Nefi kuchukua hiyo Bamba ya shaba kutoka ndani ya nyumba.

Wakati Lamani na Lemueli waliona Nefi akija ndani ya nguo za Labani, walifikiria Labani aliua ndugu yao na alikuwa akija kuwaua nao Nefi aliita msiogope ni mimi, ni mimi Nefi.

Mtumishi wa Labani aliogopa saidi, alianza kutetemeka. Aligeuka akimbie mbali lakini Nefi alimzuia na akaahidi kuacha uhai wa huyu mtu na kumpa huru kama yeye atahidi kwenda nao. Wandugu warirudi kuelekea nyikani na kujiunga na baba yao na mama ambaye waliwangojea karibu na mto. Walileta hizo bamba za shaba ambaye shirikuwa na vitabu Tano via Musa, ambavyo vilitoa taarifa ya umbaji wa ulimwengu, Adamu na Hawa na kumbukumbu ya wayahudi kutoka mwanzoni, hata kufikia mwanzo wa utawala wa Zedekia, mfalme wa Yuda. Hizo Bamba zilitoa habari ya unabii wa manabii watakatifu juu ya hiyo Bamba za shaba kulikuwa kizazi cha baba wa Lehi na alikuja kugundua ya kwamba alikua uzao wa Yusufu; aliyekuwa motto wa Yakobo, aliye uzwa kwenda Misiri, na ambaye alihifadhiwa na mkono wa Mungu, ili aweze kulinda Baba yake Yakobo na watu wa nyumba yake wote kutoka maafa ya njaa na waliongozwa kutoka utumwa na nchi ya Misiri, na yule yule Mungu ambaye aliwahifadhi.

### *Kurudi Tena Hadi Yerusalemu*

(1 Nephi 2:7-11)

Bwana alinena kwa Lehi mara nyingine, akimwambia ya kwamba jamii yake wasiende mpaka nyikani peke yao. Inawapasa kurudi Yerusalemu na kuleta jamii ya Ishmaeli pamoja nao. Ishmaeli alikua mtu mwingine ambaye alimpenda Mungu na alikuwa jamii yenye mabinti tano na vijana wawili pamoja

jamii zao wenyewe. Vijana wa Lehi watahitaji wake zao wawe na jamii watamiliki. Wale wandugu wakarudi mpaka Yerusalemu na wakamwambia Ishmaeli juu ya maono ya Lehi. Mungu akagusa moyo wa Ishmaeli na alichukua jamii yake, na kujiunga na Lehi na jamii yake katika safari yao kwenda nchi mpya.

## SAFARI KUELEKEA NCHI YA HADI

### *Liahona*

(1Nefi 5:10-12, Alma 17:71-74)



Usiku moja Lehi alivyokuwa ndani ya hema yake, Mungu alinena naye; kesho utaendelea na safari yako Lehi alishangaa ni wapi hii nchi mpya iko na ni njia gain watasafiri kuipata wakati wa asubuhi, wakati Lehi alipofungua kilango ya hema yake aliona mpira wa Bamba chini ya ardhi, kikimulika katika mwangaza wa jua wa asubuhi. Juu ya mpira kulikuwa na mishale, ilielekeza katika upande waliovyostahili kusafiri katika nyikani. Lehi aliita mpira huo Lihona, ambaye inamanisha duara.

Jamii ya Lehi na Ishmaeli, na Zoram, mtumishi wa Labani walitoka kwelekea katika safari yao, mpaka nchi mpya. Walivyo safari iyo Lahona iliwaongoza kwenye chakula na maji.

### *Kwa Njia Ndogo Mungu Alifanya Vitu Vikuu*

(1Nefi 5:17-38)

Kila wakati msafara wa Lehi uliposimaa kituoni, vijana wake walichukua upindi na mishale yao na kuondoka nje kuwinda mawindo kwa chakula chao. Siku moja walitafuta mawindo lakini hawakupata chochote na hata ingawa wangepata, hawangeichukua kwa kuwa Lamani na Lemueli upindi wao ulikuwa umepoteza chupa na upindi wa Nefi ulikuwa umevunjika. Wachovu na wenye njaa hao wandugu walirudi kituoni. Sawa kama wakati mwingi kabla, Lamani na Lemueli hawakumtumainia Mungu ama hawakumuuliza usaidizi zaidi wakawa wenye hasira. Walakini, Nefi alibaki mwaminifu na akawambia ndugu zake ni lazima waweke tumaini lao kwa Mungu.

Nefi alipata mti, akatoa kisu chake, na akatengeneza upinde mpya. Yeye alijua walihitaji msaada wa Mungu ili kupata mawindo kwa hivyo aliuliza Baba yake kuuliza kutoka kwa Mungu ni wapi wanaweza kwenda kuwinda. Lehi aliomba na tena Mungu akawambia kuangalia kwenye mpira washaba na kuona magizo yaliyo andikwa juu yake. Juu ya Lahona yaliandikwa haya maneno; Hii mwelekezi itafanya kazi tu wakati mtaomba na kunitii mimi; kama nyinyi ni waminifu nitandika neon langu juu ya laohona kuwaongoza.

Kwa njia ndogo, Bwana anaweza kuleta vitu vikubwa, Nefi aliwajulisha. Mishale iliokuwa juu ya Laohona ilichongoka kuelekea juu yam lima, kwa hivyo Nefi alivurumisha upinde wake mgongoni na

akaanza kutembea kuelekea juu mlimani. Vile Mungu alivyo ahidi, kule juu kwa mlima Nefi alipata wanyama wengi wakikula majani. Alitoa upinde wake na kurusha kwa mawindo kupata chakula mezani usiku huo.

### *Nchi Ya Utele*

(1 Nefi 5:55-67, 75-76)

Lehi na jamii yake walitembea kupitia nyikani ikwachukua miaka mingi. Kwa hofu ya kwamba watu wa Yerusalemu wanaweza kuwatafuta, hawakutengeneza moto kupikia chakula chao. Hata ingawa walikula nyama yao mbichi, Mungu aliibariki na nyama ikawa na ladha nzuri na kuwafanya wenye nguvu na afya.

Katika njiani, vijana wa Lehi na Zoramu walioa binti wa Ishmaeli. Mungu aliwabariki hawa wanawake wadogo na wakati walikuwa na watoto, wakawa na nguvu na hodari kuendelea matembezi malefu. Watoto wao walizaliwa katika nyikani. Hata Lehi na Sariah, ambaye waliendelea kuwa wakongwe, walikuwa na vijana wawili saidi, Yakobo na Yusufu.

Mwishoni baada ya miaka nane milefu wasafiri wachovu, walifika ukingo wa bahari. Hapa penyewe kando ya bahari ilijaawa na matunda na asali ya nyuki hata wakaiita nchi ya utele. Hapa kando ya bahari, walitengeneza hema zao na wakapumzika kidogo.

### *Kuunda Meli*

(1 Nefi 5:68-96, 153- 173)

Siku moja Mungu alinena kwa Nefi, akimuamuru yeye mwenyewe kuenda juu mlimani. Hapo kwenye mlima, Mungu alimwagiza Nefi jinsi ya kuunda meli watakayoitumia kuvuka bahari kuu.

Wakati Nefi alipomuuliza Mungu ni wapi ataupata madini kutengenezea vyombo vilivyo takikana kuunda meli kama hiyo, Mungu alimwonyesha ni wapi atapata mawe yaliojaa madini. Nefi aliwasha moto na kwa mivuo iliyotengenezwa kutoka ngozi ya wanyama, ulipepea moto huo kuufanya moto zaidi kama vile moto uliongezeka kuwa moto sana na kuwa juu, madini ya vyombo vienye nguvu vilotoa vingi inje mawe.

Wakati Lamani na Lemuel waliona Nefi akifanya kazi walikataa kusaidia na kuanza kunungunika, wakisema, ndugu yao Nefi hakujua vile ataunda meli na alikua anapoteza wakati wake kutengeneza vyombo. Ndugu hao pia walikuwa na uchungu mwingi juu ya kuondoka nyumbani kwao na utajiri katika Yerusalemu na kutumia miaka katika nyikani kwa sababu ya hasira yao, Lamani na Lemueli waliribu kumshinda Nefi na kumtupa ndani ya bahari kutosa majini. Nefi aliona nguvu za Mungu zikija juu yake na aliwaonya ndugu zake, katika jina la Mungu mwenyezi, ninawamuru ninyi, musiniguze, kwa vile nimejazwa pamoja na nguvu za mungu na yeyote ataniguza mimi atakufa. Lamani na Lemueli walisikia nguvu nyingi za Mungu zikinizunguka Nefi na waliogopa.

Baada ya siku nyingi, Mungu alimwambia Nefi awaguze ndugu zake. Mungu aliahidi hawatakufa lakini atawafadhaisha ili kuthibitisha nguvu zake ziko pamoja naye. Wakati Nefi alipoguza Lamani na

Lemueli, nguvu kuu za Mungu ziliwangusha mpaka kwa ardhi. Baada ya kuona nguvu za Mungu, Lamani na Lemuel walisaidia Nefi katika kuunda meli kulingana na magizo Mungu alikuwa amempa Nefi.

### *Kuvuka Bahari*

(1 Nefi 5:175-211)

Wakati Nefi na ndugu zake walimaliza kujenga merikebu, Mungu alimnenea Lehi na kumwambia ilikuwa wakati wa kuendelea safari yao. Siku iliofuata walianza kufunga merikebu na matunda, nyama asali ya nyuki ya mwitu na mbegu waliokusanya katika nyikani kwa ajili ya safari ndefu kupitia baharini. Merikebu ilika mwendo na Laohona iliwaonyesha njia wataelekea wakati Mungu alituma upepo wenye tulivu ili kusukuma merikebu kupitia baharini kwenda kwa nchi mpya.

Mara walipoondoka, Laman na Lemueli upesi walisahau ilikuwa ni Mungu ambaye aliwalinda salama juu ya nchi. Badala ya kumshukuru Mungu, walianza kujifurahisha, wakicheza ngoma, wakiimba na kuongea utovu wa adabu, kwa mwadimisho wa safari yao nzuri. Nefi aliogopa kwa ajili ya ndugu zake, kwa sababu jinsi walipotenda kwa hivyo aliwaonya kumukumbuka Mungu.

Hao wandugu walichukizwa na Nefi na kusema ndugu yao mdogo hataenda kutawala juu yao. Lamani na Lemueli walifunga Nefi kwa kamba nyembamba yenye nguvu na wakati ule kila kitu kilianza kuenda vibaya. Ile Laohona, ambaye iliwapa njia ya kwenda ilisimama kufanya kazi mawingu yakaendelea kuwa meusi na upepo mkali ukaanza kishindo, ukipiga tanga ya merikebu na kupiga merikebu kwenda nyuma kwa siku tatu. Lehi na Saria waliogopa sana kwa sababu ya uovu wa Lamani na Lemueli ivyo wakawa wagonjwa. Maombi ya kumfungua Nefi yalienda bila kujibiwa. Lamani na Lemueli hawakuweza kusikiza miguu na mkono ya Nefi ikawa vidonda na ikivimba kutokana na kamba, lakini hata hivyo alimutumaini Mungu. Dhoruba ikawa kali sana, pamoja na mawimbi makuu ya kiosha toka upande huu mpaka wa pili wa pamba ya merikebu. Kwa kila wimbi merikebu ilizama chini zaidi ndani ya maji. Kama hiyo merikebu ilipoanza kuzama, Lamani na Lemueli walilfahamu Mungu amekasirika nao walimfungua ndugu yao.

Nefi aliokota iyo Laohona. Tena, iyo dira ilionyesha njia ya kwendesha kwa tanga. Ndipo Nefi aliomba, akiuliza Mungu asimamishe hiyo dhoruba ya kuogofya. Kwa ghafula upepo ukawa tulivu na maji yakatulia. Upepo wa upole ukaanza kuvuma ukisukuma merikebu yao kwenda kwa nchi mpya yao.

## <u>KUFIKA NCHI YA AHADI</u>

### *Mfiko Kuwasiri Kwa Nchi Mpya*

(1Nefi 5:212 - 224)

Baada ya wiki nyingi kwa bahari, Lehi na jamii yake, waliona nchi katika upeo wa macho, ilikuwa nchi ya ahadi. Baada ya kufungua merikebu yao, walianza kupeleleza nchi yao mpya. Ilikuwa nchi nzuri namna

gain, pamoja na kila kitu Mungu aliahidi pamoja na wingi wa wanyama wa mwitu kuwinda na kuwafuga kwa ajili ya matumishi yao. Walijenga nyumba na kupanda mbegu walichukua kuvuka bahari.

Nchi ilijawa na mawe yenye madini na dhahabu yenye thamani. Mungu aliagiza Nefi kutunza maandiko. Nefi alikuwa mtiifu, na alitengeneza pamba ya madini kuandika juu yake. Katika hizi pamba, alitia kumbukumbu ya baba yake, safari yao kutoka Yerusalemu na unabii ambaye ulikuja kwa maagizo ya watu wake na kusudi ya busara nyingine, hiyo makusudi yalifahamika na Mungu mwenyewe.

### *Lamani Na Lemueli Waliasi*

(2Nefi 3:8-25; 2Nefi 4:1-16, 29-44; Yakobo 1:13- 14)

Miaka nyingi ilipita tangu Lehi na jamii yake kuondoka Yerusalemu na kufanya maskani yao katika nchi ya ahadi. Lehi alikuwa mzee na alijua karibuni anaweza kufa. Aliita vijana wake wote ndani akawabariki, na kuwafundisha kwa kuwa Bwana Mungu alisema ya kwamba kwa kuwa mtashika amuri zangu, mtasitawi katika nchi na kwa kuwa ninyi. Mkikosa kulinda amri zangu mtaweza kukatwa kutoka kwa uzo wangu. Haikukuwa muda mrefu baada Lehi kuwaonya vijana wake ivyo alifuriki.

Juu ya kifo cha Lehi, Mungu alichagua Nefi kuongoza watu. Kama vile walivyotenda mara nyingi nyuma Lamani na Lemueli walipata kuwa na hasira kwa hilo jambo ya kwamba ndugu yao mdogo alikuwa atawale juu yao. Hasira yao iliongezeka saidia juu ya Nefi walijaribu tena kutafuta kuchukua maisha yake.

Aaruni alimwagiza mfalme katika unyenyekevu na sikitiko; ni lazima uiname mbele ya Mungu na kuita jina lake katika imani, ukiungama dhambi zako. Kisha mfalme aliinama mbele ya Bwana na kulia; Mungu, utaweza kujijulisha mwenyewe kwangu? Nitaachilia dhambi mbali kukujua ili niweze kuinuliwa kutoka kwa wafu, na kuokolewa katika siku za mwisho.

Wakati mfalme alisema haya maneno, alishindwa pamoja na Roho wa Mungu na alianguka kwenye sakafu akiwa kama amekufa. Watumishi walikimbia kumwambia malkia.

Wakati alikuja na kuona mfalme juu ya sakafu akiwa kama aliyekufa, na Aaruni na ndugu zake wakisimama kana kwamba walikuwa chanzo ya kuanguka kwake, alikasirika pamoja nao, na kuwamuru watumishi kuwaua. Sasa watumishi walikuwa wameona chanzo cha kuanguka cha mfalme, kwa sababu hii waliogopa kuweka mikono yao juu ya Aaruni na ndugu zake na walitoa hoja kwa malkia, wakisema; mbona wewe unatuamuru sisi kwamba tuweze kuwaua hawa watu, wakati mmoja wao ni mwenye nguvu zaidi kuliko sisi zote?

Malkia aliona hofu ya watumishi naye pia alianza kuogopa maovu mengine yanaweza kuja juu yake. Aliwaamuru watumishi wake kuenda na kuiita watu, ili waweze kuwaua Aaruni na wenzake.

Aaruni aliona kusudi la malkia, na pia alijua ugumu wa mioyo ya watu, aliogopa umati utaweza kuja pamoja na kutakuwa ushindani mkuu na ghasia miongoni mwao. Aaruni aliweka mkono wake mbele na alimwambia mfalme kusimama. Mfalme alisimama juu ya miguu yake, akipokea nguvu yake machoni pa malkia na wengi wa watumishi.

Mfalme alisimama mbele ya watu na alianza kuhudumu kwao. Na alihudumu hadi kwao hata kwamba nyumba yake nzima iligeuka hadi kwa Bwana. Wakati watu walifika mfalme alisimama na aliongea kwao na pia aliamuru Aaroni na ndugu zake kusimama mbele kati ya umati kuhubiri kwao.

Mfalme alitoa tangazo kote kote nchini miongoni mwa watu wake, ya kwamba hakuna madhara yataweza kuja kwa wana wa Mosia na walikuwa huru kuhubiri popote katika nchi. Aaroni na ndugu wake walisafiri kwa miji mingi na kuanzisha makanisa kokote kwa nchi ya Walamani.

## **KUTOPATANA NA – NEFI – LEHI**

### *Kuagamiza Silaha Za Vita*

(Alma 14:17-20, 23-55)

Walamani ambao waligeuka kwa Bwana walifanya mabadiliko makuu na hawakukua watu wazembe tena. Wakawa marafiki pamoja na maadui wao wakwanza, WaNefi. Walikuwa wamebadilika kuzidi ya kuwa walitamani kupata jina ambaye litaweza kuwapambanua kutoka kwa Walamani ndugu zao. Walichagua kuitwa kutopatana na – Nefi – Lehi. Mfalme ambaye alitawala juu ya nchi yote alikuwa mzee na alijua ataweza kufa karibuni. Hivyo alitoa ufalme juu ya kijana wake na aliita jina lake kutopatana na – Nefi – Lehi.

Walamani ambao walikataa ujumbe wa Mungu, walipata kuwa wenye hasira pamoja na waumini wapia. Walikusanya jeshi la askari kuja kwa vita juu ya watu wa Mungu. Kutopatana Na – Nefi – Lehi na vijana wa Mosia walikusanyika katika nchi ya Ishmaeli kuzungumza pamoja na mfalme Lamoni kama ni nini wanaweza kufanya kulinda juu ya Walamani.

Sasa hakukuwa roho moja miongoni mwa watu wote ambao walikuwa wamegeuka hadi kwa Bwana ya kwamba waliweza kuokota silaha juu ya ndugu zao. Mfalme wao aliwamuru wasiweze hata kufanya matengenezo ya vita. Walikusanyika na kuzika silaha zao zote za vita kwenda chini katika ardhi; hapo waliweka nadhiri wata kusudia kufa kabla kuzoa visu viao tena.

Hii haikusimamisha jeshi la maskari wa Walamani kutoka kuja kwa vita. Katika nchi ya Ishmaeli, vishindo via mwendo wa Jeshi la askari ilisikika ikija karibu na karibu. Wakati jeshi la askri walifika, watu wa kutopatana na – Nefi – Lehi walianguka kwa miguu yao na walimuita Mungu. Walamani walishambulia na walianza kuua waumini pamoja na visu vyao. Wakati baadhi ya Walamani waliona ndugu zao wa kwanza wakikataa kupigana na kumsifu Mungu hata kama walikufa, mioyo yao iliguswa na walijuta kwa kitu ambao walikuwa wamefanya na kurusha silaha zao chini. Siku hiyo Walamani zaidi ya elifu waliletwa kwa hekima ya Mungu. Zaidi ya tarakimu walikuwa Walamani ambao walikuja kwa ukweli wa Mungu kuliko hesabu ya waumini ambao waliuliwa.

### *Kurejea Zarahemia*

(Alma 15:1-31)

Kwa muda Walamani waliahirisha mbali, Walakini hatimaye walirudi kushambulia watu wa kutopatana na Nefi-Lehi na walianza kuwaangamiza. Kutopatana na Neph-Lehi walikataa kuzoa silaha zao na walivumilia kuangamizwa na maadui zao. Ammoni na ndugu yake hawakuweza kustahimili kuona haya maangamizi ya ndugu wao Wapia na walisema kwa Mfalme; wacha tukusanye watu pamoja na kuteremka kwenda Zarahemia. Walakini mfalme aliogopa waNefi watakumbuka mauaji ya watu kwa kusudi wao wengi na watapenda kuwaua.

Ammoni alisema, nitaenda na kuuliza kwa Bwana. Kama atasema hadi kwetu, teremka hadi kwa ndugu wetu, hutakwenda? Na mfalme alisema kama bwana atatwaambia tuende tutatelemka mpaka kwa

ndugu wetu, na tutakuwa watumwa wao hadi tutengeneza hata kwao mauaji kwa kusudi mengi na dhambi ambaye tulikuwa tumetenda juu yao. Ammoni alimwambia mfalme; ilikuwa kushindana na sheria ya ndugu wetu, ya kwamba kutakuwa na watumwa wowote miongoni mwao, kwa sababu hii, wacha tutelemke na tutumainie juu ya msamaha, wa ndugu zetu. Mfalme alisema hadi kwake; uliza kwa Bwana, na ikiwa atanena kwetu tuende, tutaenda; kwa sababu nyingine tutaangamia katika nchi.

Ammoni aliendа na kuulizia kwa Bwana, na Bwana alinena kwake; toa watu hawa nje ya nchi hii; na wamebarikiwa watu hawa katika kizazi hiki; kwa kuwa nitawalinda. Ammoni aliendа na kumwambia mfalme maneno yote ambayo Bwana alimwonyesha.

Watu wa kutopatana na Nefi – Lehi walikusanya makundi yao yote makundi ya wanyama wakubwa, na ndipo walisafiri kwenye mpaka wa Zarahemia. Pale walingoja kwa mashaka wakati Ammoni aliendа kuongea kwa mwamuzi mkuuu wa nchi. Mwamuzi alituma tangazo katika nchi nzima akiuliza watu kama wataweza kukubali watu wa kutopatana na Nefi – Lehi kama ndugu zao na kuwapa mahali katika nchi.

Wakati Ammoni alirudi kwenye kituo cha mpaka, alileta ujumbe kutoka kwa watu wa Zarahemia. Tutawapa, ndugu wetu wapya, nchi ya Yeshoni. Tutawalinda pamoja na jeshi la askari wetu. Tunauliza peke yake kwamba mtoe chakula kwa jeshi la askari wetu. Ni furaha ipi ilikuwa miongoni mwa watu wa kutopatana na Nefi – Lehi. Walivyo kaa katika makao yao mapya katika nchi ya Yeshoni, watu wa kutopatana na Nefi – Lehi walikuja kuitwa watu wa Ammoni, au Wammoni na walitambulika kutoka wakati huo na kuendelea kwa imani yao kuu kwa Mungu, kazi yao hodari, uaminifu wao na uzuri wao kwa wote.

***Mungu Alinyamazisha Korihori***

(Alma 16:6-77)

Watu wote wa Zarahemia waliishi kwa amani kwa muda. Ndipo katika mwaka wa saba wa utawala wa waamuzi, mtu muovu alitajwa kama Korihor aliingia nchini. Alianza kufundisha kwamba unabii wa kuja kwa Kristo ulikuwa si kitu walakini mafundhisho yaliyotokea zamani ya ujinga. Aliwambia watu; fanya mnavyotaka kwa sababu wakati mtu amekufa, hiyo ndiyo mwisho. WaNefi wengi waliamini maneno ya Korihori.

Watu waminifu ambao hawakuweza kuamini uongo wa korihori walimfunga na kumleta mbele ya kuani mkuu, aliyeitwa Giddona. Kuani mkuu aliuliza Korihori; kwa nini wewe unazunguka kupotosha njia za Bwana? Kwa nini wewe unafundisha hawa watu kwamba hakutakuwa Kristo, kukatiza kufurahi kwao? Kwa nini wewe unaongea kushindana na unabii wote wa manabii watakatifu?

Na Korihori alimjibu Giddona; kwa sababu sifundishi mafundisho ya zamani ya ujinga wa baba zenu, na kwa sababu sifundishi watu hawa kujishirutisha chini sheria ya ujinga na matendo ambayo yaliwekwa chini na makuani wa zamani, kunufaika na nguvu na uwezo juu yao, kuwaweka katika kutokujua. Unasema kwamba huo unabii wa kale ni waukweli, walakini na kwambia hujui ya kwamba niwaukweli, unasema Kristo atakuja, walakini nakuambia hujui ya kwamba kutakuwa na Kristo. Na unasema Kristo atauliwa kwa sababu ya dhambi ya ulimwengu; na hivyo unaogoza hawa watu kwa mafundisho yalitokea zamani ya ujinga ya baba zenu, na kwa kupatana na tamaa yako mwenyewe.

Ndipo Korihori alipelekwa hadi nchi ya Zarahemia kuletwa mbele ya Alma, mwamuzi mkuu. Korihori alisema sana kwa maasi juu ya Alma; unafundisha kuhusu Kristo tu kuwaweka watu chini utawala wako.  Unatulia chini wakati wanafanya kazi, ndipo unachukua pesa zao.

Hii ilikuwa uwongo; Alma hajawai kuchukua pesa kwa kumtumikia Bwana walakini alikuwa kila mara akifanya kazi kwa mikono yake mwenyewe kujitegemea.  Hapo Alma aliuliza Korihori, unaamini kuna Mungu? Korihori alijibu; Hapana! Walakini Alma alijua fikira za moyo wa Korihori na ya kwamba aliamini.

Alma alizungumza kwa Korihori; na sasa, ni ushahidi gani unaye kwamba hakuna Mungu, au ya kwamba Kristo hatakuja? Nakwambia huna ushahidi, isipokuwa neno lako pekee.  Nina vitu vyote kama ushuhuda ya kwamba vitu hivi ni vya ukweli; na wewe pia una vitu vyote kama ushuhuda kwako kwamba ni vya kweli; na utavikana? Umepagawa na roho ya uwongo, na umeondoa Roho wa Mungu, ya kwamba asiwe na mahali ndani yako; walakini shetani ana nguvu juu yako, na anakuchukua huku na huku, ukifanya matengano, kwamba aweze kwangamiza watoto wa Mungu.

Korihori alinena; nitakana, isipokuwa utanionyesha ishara kwamba niweze kusadiki kuna Mungu na ako na nguvu, na hapo nitasadiki kwa ukweli wa maneno yako.

Alma alihuzunishwa kwa sababu ya ugumu wa moyo wa Korihori na ya kwamba alipinga Roho wa ukweli.  Alma alimwambia Korihori itakuwa afadhali kwamba moyo wake ungeweza kupolea, kuliko aweze kuleta mioyo mingi chini kwa uharibifu na uwongo na maneno ya kujipendekeza.

Kwa sababu hii kama utakana tena, Alma alimwambia Korihori, Mungu atakupiga sana, na atakupiga kuwa bubu, na kamwe utafungua kinywa chako zaidi, hata hatadanganya watu hawa kwa vyovyote.  Sasa wakati Alma aliyasema haya maneno, Korihori alipigwa kuwa bubu.

Alma alikabidhi Korihori barua, Mungu amekuonyesha Ishara, je unaamini? Korihori alimwandikia, shetani aliniingilia katika mfano wa malaika.  Aliniambia niende kukusanya watu wale wanaomfuata Mungu asiojulikana.  Tafadhali uliza Mungu aondoe laana hii kutoka kwangu.

Alma alijua kwamba kama Korihori ataweza kuongea tena ataweza kurudi kwa njia zake za zamani na kufundisha uongo wake tena kwa hivyo laana haikutolewa kutoka Korihori.  Wakati wafuasi walimwoona, walijua alikuwa ameadhibiwa kwa uongo wake na walirudi kwa Bwana.  Korihori aliondoka Zarahemia na alienda nchi nyingine.  Alienda kutoka nyumba kwa nyumba akiomba pesa mpaka siku alikanyagwa kufa na kikundi cha watu wenye hasira.  Na hivyo tunaona mwisho wake ambaye aligeuza njia za Bwana; na hivyo tunaona kwamba shetani hawezi kusaidia watoto wake katika siku za mwisho, walaki kwa haraka anawavuta chini jehanum.

## *Waamini Wanyenyekevu*

(Alma 16:78-134, 175-181, 219-222, 242-250)

Mara moja baada ya kusikia kifo cha Korihori, Alma alipata habari ya kwamba mtu mwingine aliyeitwa Zoramu alikuwa anajaribu kuangamiza kanisa.  Sasa Zoramu aliongoza kikundi cha watu kwenye nchi ya Antionumu kuanziza kanisa mpya katika hii ataweza kufundisha mafunzo ya uongo.  Alma alihitaji kuokoa

watu ambao sasa walijiita Wazoramu, hivyo Alma, wawili wa vijana wake na baadhi ya makasisi walienda kwenye nchi ya Antionumu kuhubiri.

Wakati watu walifika Antionumu waliona kanisa ya fahari Wazoramu walikuwa wamejenga. Katikati ya kila kanisa ilikuwa jukwaa la heshima waliita Rameumptoni. Hii Rameumptoni ilikuwa kubwa pekee kuchukua mtu mmoja. Watu walienda kanisa wakijivika katika nguo nzuri na walijipamba pamoja na dhahabu na fedha. Wakati wa ibada ya kanisa mtu mmoja kwa wakati aliweza kupanda kwenye Rameumptoni. Aliweza kuinua mikono yake juu na kusema maombi sawa harisi; ho Mungu tunakushukuru kwa kututenga sisi kutoka ndugu zetu. Tunakushukuru kwa kutuchagua kuwa watu wamaana ambao hawaamini katika mawazo ya ujinga kwamba Kristo anakuja. Tunashukuru ya kwamba tunaenda kuokolewa wakati wote wanatuzunguka wanaenda jehanamu. Baada ya watu kutoa maombi yao walirudi kwa makao yao na kamwe hawakuongea juu ya Mungu tena hadi wakati wakukusanyika mara nyingine.

Wakati Alma aliona hii moyo wake ulisikitika. Aliweza kuona hawa watu wa Antinumu waliongea kwa Mungu pamoja na vinywa viao, walakini hawakujali juu yake katika mioyo yao. Walijali tu juu ya nguo zao nzuri na kwa vitu na dhahabu. Mungu alimpa Alma na makasisi wengine nguvu ya Roho yake kuhubiri kwa Wazoramu. Walitengana na kuenda kote kote nchini wakifundisha katika makwao na kuhubiri katika makanisa.

Siku moja vile Alma alikuwa akiongea juu ya kilima kiliyoitwa Onida, umati kuu wa watu walikuja kwake, na wengi wao walikuwa maskini. Mmoja wa viongozi wao miongoni mwa watu maskini alimwambia Alma ya kwamba kwa sababu walikuwa maskini, makuani hawakuweza kuwaruhusu katika kanisa. Hatuna mahali pa kuabudu Mungu, walisema; tutafanya nini?

Wakati Alma aliangalia kwenye nyuso za watu hawa maskini alifurahi. Aliweza kuona walikuwa wamenyenyekezwa na taabu zao. Walikuwa tayari kusikia injili ya ukweli. Alisimamisha kuongea kwenye umati wote na alizungumza tu kwa hawa watu maskini.

Sasa wakati Alma alisikia haya alisema; mnafikiri mnaweza tu kumuabudu Mungu siku moja kwa week penye kanisa? Mnaweza kuomba katika nyumbani kwenu, katika mashamba yenu na mmea, kwa jamii zenu na juu ya nguvu ya shetani. Ni vyema ya kwamba mmetupwa nje ya makanisa yenu, ili muweze kuwa wanyenyekefu, na ili muweze kujifunza maarifa; kwa sababu lazima ya kwamba mnatakikana kujifunza maarifa. Ni kwa sababu mmetupwa inje, ya kwamba mmedharauliwa na ndugu zenu, kwa sababu ya umasikini wenu kuwa zaidi mmeletwa katika unyenyekevu wa moyo; maana kwa lazima mmeshushwa kuwa wanyenyekevu, na sasa kwa sababu mmeshurutishwa kuwa wanyenyekefu, heri ninyi, kwa maana mtu awezapo, kama ameshushwa kuwa mnyenyekefu, anaomba toba. Na sasa kama vile nilisema kwenu, kwa sababu mlishushwa kuwa wanyenyekefu, mlibarikiwa. Hamfikiri ya kwamba wamebarikiwa zaidi wale kwa kweli wamejinyenyekea wao wenyewe kwa sababu ya neno? Ye yote kwa kweli ananyenyekea mwenyewe na kutubu dhambi zake na kuvumilia hadi mwisho, sawa naye atabarikiwa; hata amebarikiwa zaidi sana kuliko wale wote ambaye wameshushwa kuwa wanyenyekefu, kwa sababu ya kuzidi umaskini wao. Wamebarikiwa wale wote wamenyenyekea wao wenyewe, bila kushushwa kuwa wanyenyekefu, kwa

maneno mengine; amebarikiwa yule ambaye anaamini neno la Mungu, na amebatizwa bila ushupavu wa moyo.

Watawala na makuani walikuwa wenye hasira sana kwa sababu walijua wanaweza kupoteza nguvu zao kama watu watafuata Alma. Baada ya Alma na ndugu zake kurudi mpaka Jershon, viongozi wa Wazoramu walienda pande zote kwa siri wakiuliza watu kama waliamini katika maneno ya Alma. Wale ambao waliamini walitupwa nje ya nchi. Watu wazuri wa Yason walikumbuka jinsi gain ilikuwa kuacha nchi yao hata walifahamu wazoramu.

### *Vita Pamoja Na Wazoramu*

(Alma 16:247-255; Alma 20:17-100; Alma 21:1-2]

Wazoramu waovu hawakuridhika kwa kulazimisha watu wa washindana na Nefi-Lehi kuondoka katika nchi. Shetani alichochea hata hasira saidi katika mioyo yao na wazoramu waliungana pamoja na walamani kuja vitani juu ya nchi ya Yasoni. Nchi ya Yasoni ilikuwa juu ya mpaka wa ufalme wa walamani na ilikuwa ni mahali rahisi ya kushambulia.

Wakati watu wa Yasoni waliona wazoramu na walamani wakijiandaa kwa vita, walikimbia mpaka sehemu nyingine ya nchi. Wanajeshi wa waNefi walisogea kuingia Yasoni na wakijiandaa kupigana na walamani katika mapigano. WaNefi walikuwa tayari kwa mapigano kwa kuwa walifuata afisa mkuu wao, mtu wa miaka ishirini na tano aliyeitwa Moroni.

Ilikuwa katika mwaka wa kumi na nne wa utawala wa wamuzi; walamani walikuja juu ya waNefi kwa mapigano na walamani walivikwa katika kipande jembamba cha nguo. Nia ya kwanza ya wanajeshi wa waNefi walijaza mioyo yao na uoga. WaNefi walivikwa nguo nzito na kipande cha pamba kifuani. Kumetameta katika jua ilikuwa nyingi, labda maelifu ya ngao ya chuma. Kiongozi wa wanajeshi wa walamani, mtu anayeitwa Zerahemna, aliamuru watu wake kubadili mwendo na kushambulia sehemu nyingine ya nchi.

Wanajeshi wa waNefi walikuwa na kitu Fulani hata chenye nguvu kuliko kipande cha pamba kifuani na ngao ya kuwalinda; walikuwa na nguvu za Mungu. Walikuwa wamefundishwa na Mungu ya kwamba hawakuanziza vita walikuwa na haki ya kulinda kanisa yao, jamii yao na ardhi yao. Mungu aliwambia waNefi ni wapi walamani walikuwa wamepanga kupiga. Kama vile walamani walijiandaa kushambulia waliona wamezungukwa na wanajeshi wa Moroni walamani waliogofya.

Wakati Moroni aliona vile wanajeshi wa Zerehemna waliogopa, aliamuru jeshi lake kusimamisha vita. Moroni alimuita Zerahemna; hatutaki kukuua wewe, unaweza kuona ya kwamba nguvu za Mungu ziko pamoja nasi. Hii ni kwa sababu ya imani yetu kwa kristo. Ahidi usipigane nasi na tutakufanya huru.

Zerehemna aliacha kisu chake lakini wakati Moroni aliona hii alisema zitakufanya huru wewe isipokuwa utoe ahadi kutokuja kwa vita juu yetu tena. Zerahemna aliokota kisu chake na kuamuru askari wake kupigana. Baadhi ya askari hawakupigana lakini wengine walisimama pamoja na Zerahemna na

walianza kupigana mara nyingine. Wakati Zeremna aliona ya kwamba karibuni watu wake wote watauliwa, alijisalimisha na akafanya maagano ya amani. WaNefi walishangilia na kutoa shukrani kwa Mungu kwa kuwalinda kutoka maadui zao.

### *Jina La Heshima La Uhuru*

(Alma 21; 3-7, 16-72)

Siku moja Alma, kuani mkuu aliita vijana wake kwake, Helaman kijana wangu, jukumu ya kuweka maandiko matakatifu sasa ni yako. Kumbuka kijana wangu, baraka na laana ya nchi hii. Wote ambao wanaishi hapa watabarikiwa kama watamtumikia Mungu, lakini laana kama watarudia uovu.

Baada Alma kusema kwaheri kwa vijana wake na watu wake, aliwaacha kuhubiri injili ya kristo pote pote nchini na haikusikika kutoka kwake tena. Wengine katika nchi waliamini ya kwamba kwa sababu ya wema mkuu wa Alma yeye hakukufa, lakini alichukuliwa moja kwa moja kwa mungu.

Helamani na vijana wengine wa Alma walianza kufundisha na kutia nguvu kanisa. Watu wa Zerahemla walipata kuwa wenye usitawi sana na kwa huzuni, wengine wao walipata kuwa na majivuno ya utajiri wao na walisahau Mungu. Wakati Helamani na wahubiri wengine walihubiri kwao, waligeuka mbali na hawakuweza kusikia. Mtu muovu aliyeitwa Amalickia aliwachochea hawa watu wenye majivuno, akiwambia kama mtanifanya mfalme, nitawapa nguvu. Wengi waliacha Mungu na kanisa na kufuata Amalickia.

Mkuu wa askari Moroni alilazimika kusimamiza Amalickia, kutoka kuharibu uhuru wao. Akirarua kipande cha koti yake Moroni aliandika juu yake; kwa ukumbusho wa Mungu wetu, dini yetu na uhuru, na amani yetu, wake wetu na watoto wetu. Moroni alifunga kipande kilichopasuliwa cha nguo juu mwishoni mwa paona akaiita jina la heshima la UHURU. Ndipo Moroni aliinama katika nchi; katika maombi makuu; Eh, Mungu, bariki na kutulinda kama kikosi cha wakristo kinasalia katika nchi. Moroni ndipo aliendelea mbele miongoni mwa watu, akifunga jina la heshima la uhuru na kutangaza; ye yote anapenda kupigana katika nguvu za bwana, wacha wao waingie katika maagano. Wakristo waliwapokonya visu viao na walikuja wakikimbia walifanya maagano kwa kurarua koti zao kama vile Moroni alikuwa amefanya na kutupa vipande vya nguo zao waliopasua kwa miguu ya Moroni.

Watu walipiga kelele; kama sisi tutavunja sheria za Mungu wacha sisi tupasuliwe kama vile hizi nguo. Moroni alienda katika nchi na kukusanya wote ambao walikuwa wanapenda kusimama juu ya Amalickia.

Wakati watu wa Amalickia waliona hao walikuwa wengi kuwaliko, walikimbia upande wa nchi ya Nefi mahari walamani waliishi. Moroni alijua kama Amalickiah atajiunga na walamani yeye anaweza kuchochea walamani kufanya vita tena. Wanajeshi wa Moroni waliwasimamisha wafuasi wa Amalickia na kuchukua wengi wao mateka, lakini Amalickia haliokoka pamoja na wachache wa wanaume wake.

Katika nchi ya Zerahemla, kupepea kutoka urefu juu ya kila mnara kulikuwa na jina la heshima la uhuru na kulikuwa na amani mara nyingine tena katika nchi.

### *Moroni Akijiandaa Kwa Vita*

(Alma 21:78-186, Alma 22:1-24)

Huku waNefi wakiishi kwa Amani, Amalickia alikuwa anachukua pole pole juu ya nchi ya Nefi mahali walamani waliishi. Kwa udanganyifu wake na mauaji, Amalickia akawa mfalme wa walamani. Amalickia alitaka hata nguvu nyingi, alitaka kuwafanya waNefi watumwa wake, hata kama mfalme mpya alichochea walamani kufanya vita na waNefi.

Wakati Amalickia alikuwa akiwadanganya walamani, Moroni alikuwa anatayarisha watu wake kwa vita. Alifanya kila mji wa mNefi kuingia mji uliojengwa maboma, kw kufanya jungu kuu ya taka kando kando yao. Moroni hakupenda kumwaga damu lakini alikuwa na nia ya kupigana kama atalazimika moyo wake ulikuw umejaa shukrani kwa Mungu kwa ajili ya baraka nyingi zilipeanwa kwa watu wa Zerehemla. Alikuw na imani kuu ya kwamba kama waNefi watatii amri za Mungu anaweza kuwalinda wao kwa kuwaambia wakati wa kukimbia na wakati wa kupigana.

Wakati walamani walishambulia walishangaa kuona miji ya WaNefi haikuweza kusindwa. Kama vile walamani walijaribu kuingia kwa miji juu ya mafungu makuu ya takataka, waNefi waliwafukuza pamoja na mishale na mawe. Zaidi ya walamani elfu waliuwawa ingawa wengine wa WaNefi walipata majeraha, hakuna mmoja wao alipoteza maisha yake. Wakati askari wa walamani waliona Afisa wao mkuu ameuwawa, walikimbia mpaka nyikani. Wakati walikuja kwa mfalme Amalickia walimuambia kuhusu kushindwa kwao, alihusunika sana na kumlaani Mungu hapo aliapa kumuua Moroni.

Wakati Amalickia alikuwa anamlaani Mungu, WaNefi walikuwa wanamshukuru YEYE kwa kuwaokoa kutoka kwa maadui zao. WaNefi walisitawi na walianza kujenga miji. Mji mmoja mkuu uliitwa kwa jina la mkuu wa Askari wao mpendwa Moroni. Je ni mwenye rehema na haki Mungu alikuwa kwa watu wake ulikuwa wa furaha nyingi miongoni mwa WaNefi tangu siku za Nefi wakati walikuwa wameongozwa mpaka hii nchi ya ahadi hata muda mrefu uliopita.

### **Kushinda Watu-Wamflame**

(Alma 22:38-44, Alm 23:1-44)

Katika mwaka wa ishirini na tano wa utawala wa wamuzi, pahorani alikuwa mwamuzi mkuu wa nchi. Alikuwa mzuri na mwamuzi mwenye haki. Katika mwaka huo kikundi kidogo cha watu walitaka kupadilisha sheria za haki za WaNefi. Walikuja kwa pahoran pamoja na malalamiko yao lakini pahorani alikanusha; sheria zetu sitasimama.

Hawa waasi walikuwa na huzuni sana ya kwamba walitaka kupindua serikali na kuweka mfalme, na walijiita wao watu – wamfalme. Watu ambaye walitaka kulinda sheria ile iliwafanya kuwa huru kumwabudu Mungu walijiita watu huru. Shauri ilitolewa kuamua kama waweza kuwa na mfalme ama la. Shauri la watu huru ilishinda; hakutakuwa na mfalme na pahorani alibaki katika kiti cha hukumu.

Watu wamfalme walikuwa matajiri na watu wa majivuno ambaye walitaka mamlaka juu ya wengine. Hii ilikuwa wakati mbaya sana kuwa na huu ugomvi ndani ya nchi kwa kuwa Amalickia alikuwa tena

kuchochea walamani kwa mapigano. Wakati watu-wamfalme waliarifiwa walamani walikuwa wanakuja walifurahi na kusema; hatutapigania kwa Pahorani, wacha serikari yake ianguke chini.

Wakati Moroni aliona watu alikuwa amepigania kwa ugumu zaidi kuwalinda, hawakuweza kushindania nchi yao alihuzunika sana. Alituma mjumbe kwa Pahorani nipe mamlaka nifanye hawa watu-wamflame wasaidie nchi yao. Pahorani alituma ujumbe kwa Moroni kumpa hii mamlaka. Wanajeshi wa Moroni walienda taratibu juu ya watu-wamfalme na elfu nne ya watu-wamfalme waliuliwa. Waliosalia watu-wamfalme walikubali kujiunga pamoja na ndugu zao ambao walikuwa wanapigana kwa ushujaa kwa nchi yao.

### *Vijana Helamani Elfu Mbili*

(Alma 22:27-33; Alma 23:40-41; Alma 24:63-79; Alma 26: 1-66)

Muda Moroni alikuwa mwenye shughuli ya kupiga watu - wamfalme walamani waliweza kushambulia na kushinda miji mingi. Amalickia aliuliwa na ndugu yake Amoroni alichukua amri juu ya wanajeshi wa walamani. Chuki yake ilikuwa kuu kama ile ya ndugu yake kwenda kwa WaNefi.

Wakati watu wa Ammon waliona wandugu zao WaNefi wakipigana na kufa kwa ajili yao walikuwa karibu kuchukua visu viao tena. Wakati Helamani aliona hii, aliwakomesha; mlifanya nadhiri kwa Mungu kutochukua silaha za vita kumwaga damu.

Vijana wa Waammoni walichukua hatua mbele; hatujachukua nadhiri ambaye mababa zetu walichukua na tutapigana kulinda uhuru wetu. Hawa vijana elfu mbili (2000) waliuliza Helaman kuwa kiongozi wao na walimfuata mpaka vitani. Ingawa hawajawai kupigana zamani, walipigana na ushujaa mkuu na hawakuogopa kupigana ama hata kufa. Mama zao waliwafundisha wao ya kwamba kama wataweka imani yao kwa Mungu kwa kusudi yeye ataweza kuwaokoa wao. Mungu aliwalinda na hapana mmoja wa vijana hodari elfu mbili (2000) wa Helaman walioanguka katika vita.

### *Kulindwa Katika Duara Ya Moto*

(Helamani 2:32-118)

Helaman alikuwa na vijana wawili wake mwenyewe aliwaita Lehi na Nefi. Wakati Helaman alichakaa na kufa, kijana wake, Nefi alichukua mahari yake kama mwamuuzi mkuu katika nchi. Nefi alikuwa mzuri na mwamuzi mwenye haki. Kwa sababu ya utajiri wao mwingi, watu walipata kuwa na majivuno zaidi na waasi katika mwaka wa hamusini na saba wa utawala wa wamuzi walamani waliwashambulia tena. Kwa sababu ya ouvu wao, WaNefi walipata kuwa dhaifu sana ya kwamba walamani waliwashinda hata nchi kuu ya Zarahemia. Huu kupotea wa kuogofya haungetendeka kama waNefi hawangepata kuwa na majivuno saidi. Walikuwa wamesahau ya kwamba ilikuwa ni Mungu ambaye aliwapa uwezo wao. Nefi alikumbuka maneno ya baba yake, Helaman ambaye alisema; nimewapa ninyi, vijana wangu, majina ya baba zenu wakwanza katika hii nchi. Wakati mnapokumbuka majina yao pia kumbuka kazi yao nzuri. Kumbuka vile Mungu aliwabariki wao.

Nefi alipeana kiti chake cha hukumu kwa aliyeitwa Cezoramu. Nefi na ndugu yake, Lehi, walitoka mpaka nchi kutoka mji hadi mji wakihubiri na kufundisha, wakijaribu kuleta watu wao kurudi nyuma kwa Mungu. WaNefi wengi waliamini na kuungama vile vile walamani elifu nane ambaye walitubu na walibatizwa.

Kutoka hapo Nefi na Lehi walienda mpaka nchi ya Nefi, mfalme wa walamani, pale walishikwa na kupelekwa gerezani kwa siku nyingi bila chakula. Siku moja walamani walikuja kuua wafungwa wao lakini kabla ya kuweza kufanya, Mungu alizingira Nefi na Lehi pamoja na mviringo wa moto.

Walamani waliogopa kuja karibu nao ingawa Nefi na Lehi walikuwa wanasimama katikati ya moto, hawakuweza kuchomeka. Hii iliwapa ushujaa mwingi na walianza kuhubiri kwa walamani. Waliwambia, msiogope, Mungu anawaonyesha nguvu zake nyingi. Wakati walipoyasema haya maneno, nchi na ukuta wa gereza ulianza kutikisa na mawingu meusi yalifunika gereza.

Kama vile walamani walitikiswa pamoja na hofu, sauti iliongea, tubuni ufalme wa mbinguni umekaribia, msijaribu kuangamiza watumishi wangu. Hii sauti haikukuwa yenye sauti kuu lakini ilikuwa sauti ya upole isiojongea, walakini wakati ilisungumza ulimwengu ulitetemeka. Mara tatu sauti iliongea na walamani walikuwa na hofu zaidi hawakuweza kusonga.

Katika nchi hii palikuwa na MNefi aliyeitwa Aminadab ambaye aliacha nchi yake na kuishi pamoja na Walamani. Wakati Aminadabu aliangalia kwa Nefi na Lehi aliona meka juu ya nyuso zao walipokuwa wakiongea upande wa mbinguni. Aminadabu alilia kwa umati, wangalie na walipofanya hivyo wao pia waliona nyuso zilionekana zinametameta za Nefi na Lehi na kuongea mbinguni. Walamani walistaajabu ni nani WaNefi walikuwa wakizungumzia na hapo waliuliza; tutafanya nini ili kufanya hili wingu la giza kutuacha sisi?

Aminadab siku moja alikuwa mshiriki wa kanisa la Mungu na alikumbuka vitu alikuwa amefundishwa. Aminadab aliwajibu; ni lazima utubu na kulia kwa sauti. Lia mpaka uwe na imani katika kristo. Walimlilia Mungu na giza iliondolewa na tena wao walizingirwa na nguzo la moto na waliona furaha kuu ya roho wa Mungu.

Sauti ilinena tena; Amani iwe kwenu kwa sababu ya imani yenu katika mwana wangu. Watu waliangalia juu na malaika walishuka kutoka mbinguni na kuwatumikia. Watu mia tatu waliona huu muujiza kuu siku hiyo na walienda pote pote inchini wakiambia kila mmoja kile waliona na kusikia. Karibu Walamani wote waliwaamini. Waomini waliacha silaha zao za vita na kuwarudishia WaNefi inchi walioyoishinda. Walamani walikuwa na nguvu zaidi katika imani yao hata wakapata kuwa wenye haki zaidi kuliko WaNefi. Wengine wao hata walienda kwa inchi ya WaNefi na kuwashududia juu ya Mungu. Sasa ilikuwa mwaka wa sitini na mbili (62) wa utawala wa wawamuzi na Walamani na WaNefi waliishi katika amani na mmoja kwa mwingine.

Nefi alisafiri mbele hadi inchi ya upande wa kaskazi kuhubiri watu pale.

**Muamuzi Anauliwa Kwa Kusudi**

(Helamani 3:1-24, 32-42, 63-90, 96-112)

Kwa mwaka wa sitini na saba wa utawala wa waamuzi, Nefi alirejea kwa inchi ya Zarahemia. Alishtuka kupata huku watu wamemsahau kabisa Mungu. Walikuwa wamerudia kupenda fedha, saidi hata walikuwa na nia ya kunyanganya ama kuua kuzipata. Wengi wa WaNefi walikuwa wameungana na kikundi cha siri cha wezi walioitwa wezi wa Gadianton hata wengine wa waamuzi wakuu katika inchi waliunga cheo cha wezi.

Nefi alishindwa kwa huzuni kwa maana ya dhambi za watu wake na alipanda juu ya mnara na alianza kulia na kuomba kwa watu wake. Hata vile makutano walivykusanyika kuona chanzo cha hii sikitiko kuu alizungumza kwao; Mungu ameniambia yakwamba kama hamtatubu miji yenu itapotea na ninyi nyote mtaangamizwa.

Muamuzi mkuu aliudhika na Nefi na alijaribu kupata watu kumua Nefi, lakini wengi waliogopa kumgusa. Hapo Nefi aliwambia umati; Mungu amenionyesha mimi kwamba muamuzi wenu mkuu ameuliwa na ndugu yake mwenyewe, mmoja wa wezi wa Gadiantoni. Nenda na mkaone mtampata.

Watu watano walienda kuona kama maneno ya Nefi ni ya kweli. Hapo walimpata muamuzi mkuu ameuliwa na walishikwa na hofu na kuanguka. Wakati wanaume watano waligunduliwa wakiwa kifudifudi juu ya ardhi na muamuzi mkuu amekufa, waamuzi waovu walimlaumu Nefi ya kwamba walifanya shauri pamoja na hawa wanaume kumuua muamuzi kuwafanya wao wadhanie alikuwa nabii.

Nefi aliwambia waende mpaka kwa nyumba ya ndugu wa muamuzi aliyekufa. Hapo watapata damu juu ya vazi lefu lake. Nefi aliwambia wao; wakati mtamuuliza ikiwa yeye alimuua ndugu yake, yeye ataanza kutetemeka. Yeye atakubali ya kuwa alimuua ndugu yake.

Waamuzi walituma watu kwa nyumba ya ndugu wa muamuzi mkuu. Sawa kama vile Nefi alivyosema, alikubali kumuua ndugu yake. Baadhi yao waliamini kwa sababu ya hii ishara kuu, wakati wengine walifanya gumu mioyo zao na kukataa kuamini. Nefi alienda nyumbani kwake siku hiyo akiwa na huzuni moyoni kwa dhambi ya watu wake.

### *Mungu Alituma Njaa*

(Helamani 3:113-132; Helamani 4:1-25)

WaNefi wengi walikuwa wamezidi mno kwa dhambi na hawakupenda kusikia mahubiri ya Nefi. Mioyo zao ilijaa na machukizo walianza kupigana na kuuana. Wezi wa Gadiantoni walikuwa na nguvu nyingi katika inchi kwa sababu ya dhambi ya watu.

Nefi alipokuwa akiwaza kwa huzuni kuhusu uovu wa watu wake, Mungu alisema; Nefi utabarikiwa kwa sababu umetangaza neno langu. Umeshuhudia hata wakati umechoka ama wakati wamajaribu kukuua. Kwa sababu hii maombi yako yatajibiwa. Moyo wa Nefi ulijazwa na ujasiri na alirudi kuwahubiria watu.

Wakati wa mwaka wa sabini na mbili wa utawala wa waamuzi, Nefi aliomba; ee Bwana, usiache hawa watu wangamizwe kwa kupigana, wacha iwepo katika nchi kuwafanya wakukumbuke.

Mungu alimjibu maombi ya Nefi na kwa muda mrefu mvua iliacha kunyesha, kulazimisha mazao yote kukauka. Sehemu ya maovu mengi katika nchi, watu wengi walikufa. Vita ilisimama kwa vile watu walichukua wakati wao kutafuta chakula. Kuona kuwa kweli walikuwa karibu kufa kwa kukosa chakula,

walikumbuka Nefi na kwamba alikuwa mtu wa Mungu. Waamuzi walikuja kwa Nefi kuomba; tafadhali uliza Mungu akomeshe njaa hii ili tusishindwe na njaa zote. Nefi aliweza kuona walikuwa wamenyenyekea kwa kweli na kugeuka kutoka kwa dhambi zao. Hata walikuwa wamefukuza nje wezi wa Gadiantoni. Nefi aliomba mara nyingi kwa niaba ya watu: ee Bwana kwa sababu ya unyenyekevu wao; unaweza kusamehe hawa watu na ufanye muvua irudi kwa nchi yetu.

Bwana akajibu maombi ya Nefi na kusamehe watu waliokuwa waovu zamani na kutuma mvua kunyesha juu ya nchi yenye kiu. Mara moja matunda yalinin'ginia kutoka kwa miti na nafaka na ngano ndefu ilisimama katika mashamba. Watu walifurahi na kumshukuru Mungu. Walimheshimu Nefi na ndugu yake Lehi kama watu wa Mungu. Miaka sabini na sita ya miaka ya utawala waamuzi uliisha kwa amani.

# *MLANGO WA SITA*

# KUJA KWA KRISTO KATIKA NCHI MPYA

## MANABII WALITANGAZA KUJA KWA KRISTO

***Samuel Mulamani***

**(Helamani 4:30-41; Helamani 5:1-82)**



Kwa miaka michache WaNefi na walamani waliishi kwa amani; mara nyingine tena wakawa wenye majivuno. WaNefi wengi waliasi juu ya waamuzi na kuungana na walamani wasioamini. Wezi wa Gadiantoni walitokea tena katika nchi na kuendeleza unyanganyi na mauaji. Wezi hawa wakawa wenye nguvu sana hata walikuwa wanasimama kushindana na askari wa Nefi na walamani. Katika mwaka wa themanini na sita wa utawala wa waamuzi, WaNefi walipata kuwa waovu zaidi, lakini walamani waliogeuka bado walimutumikia Mungu kwa uaminifu.

Mungu alituma Samueli, mlamani nabii kuwaonya WaNefi. Aliwatabiria; tazama mimi ni Samueli, mlamani, na ninazungumza maneneo ya Bwana ambaye ameyatia ndani ya moyo wangu; na Mungu ameyaweka katika moyo wangu kuambia watu hawa ya kwamba upanga wa haki unataka kuja juu ya watu hawa na miaka mia nne haitapita hata upanga wa haki uanguke juu ya watu hawa. Hakuna kitu kitaokoa watu hawa ila iwe kutubu na imani kwa Bwana yesu kristo. Huyu Yesu Kristo atakuja ulimwenguni na kutendewa vitu vingi; na kuuliwa kwa watu wake. Kwa hivyo Bwana asema; kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya watu wa WaNefi isipokuwa watubu nitachukua neno langu kutoka kwao, na nitaondoa Roho wangu kutoka kwao, na nitageuza mioyo za ndugu zao juu yao; nitawafanya hata kuweza kupigwa sana na upanga, na njaa, na pamoja maradhi ya kuambukiza. Nitawahukumu katika hasira yangu kali, na madui wa

kizazi cha nne wataona uharibifu wao. Kwa hakika hii itakuja isipokua mtubu. Kama mtatubu na kurudi kwa Bwana Mungu wenu, nitageuza hasira yangu. Wamebarikiwa wale ambaye watatubu na kurudi kwangu. Lakini ole kwa yule ambaye hatatubu.

Samueli alihubiri kwa siku nyingi huku Zarahemia. Mambo yake yalifanya watu kukasirika na walijaribu kumfukuza nje ya mji wao. Samueli alipokuwa akitembea kutoka Zarahemia alifikilia jinsi gani watu watakataa kusikiliza mashauri. Mungu ndipo akasungumza kwake; Samuel rudi mpaka Zarahemia nitakupa maneno utakayoyasema.

Samueli alirudi Zarahemia na alipanda juu ya ukuta wa mji. Toka pale alihutubia watu tena; Watu wa Zarahemia, Mungu amenituma niwambie mtubu kama sivyo vitu vya kuogofya vinaenda kutendeka.

Umati ulivyoanza kukusanyika karibu na ukuta wa mji, Samueli aliwambia; mnapenda fedha .zaidi kuliko Mungu. Kama hamtabadilika; nchi yenu itajaa na wezi kama mtaacha kitu chini kwa ardhi kitakuwa kimeenda asubuhi kwa sababu mtu atakuja na kuiba.

Samueli alitabiri juu ya Kristo; kwa miaka tano Yesu Kristo mwana wa Mungu anaenda kuzaliwa katika ulimwengu. Usiku atakayezaliwa jua itaghala lakini mbingu kutakuwa na mwangaza na nyota mpya itaonekana juu mawinguni. Bwana Yesu Kristo atakuja na kuteswa vitu vingi. Atakufa kwa dhambi za watu wake. Kwa wakati wa kifo chake Mungu atatuma dhoruba ya kuogofya na tetemeko la nchi, mbaya saidi ya zile umewahi kuona. Kwa siku tatu wala jua, ama mwezi ama nyota itangaa na nchi itafunikwa katika giza. Tazama ishara hizi.

Wengine wa watu waliamini mambo juu ya Samueli na walikumbuka mafunzo ya Nefi wengine wa watu hawakupenda kusikiza. Waliongezeka na hasira na walitaka kumuua Samueli walitupa mawe kwake na walirusha mishale, lakini Samueli alipoona kwa uwezo wa Mungu, aliruka chini kutoka kwa ukuta na kurudi kwa nchini yake. Hakuonekana tena katika nchi ya Zarahemia. Watu wachache wanyenyekevu ambao waliamini mambo ya Samueli walikutanika pamoja na Nefi ambaye aliwafundisha kuhusu Mungu.

## *Mwokozi Amezaliwa*

(3Nefi 1:1-24)

Nefi aliondoka katika nchi na hakuna yeyote alifahamu mahali alipokwenda na kijana wake, ambaye pia aliitwa Nefi, sasa walitunza habari iliowekwa kwa ukumbusho. Alikuwa mtu wa Mungu kama baba yake. Kama vile wakati wa kuzaliwa kwa mwokozi ulivyo karibia, Mungu alionyesha ishara nyingi na maajabu. Walakini, shetani alifanya mioyo migumu ya wasioamini na walianza kudhihaki wale ambao waliongojea kwa uaminifu kwa ishara ya kuzaliwa kwa mwokozi wao. Mara moja miaka mitano ilikuwa imepita na ilikuwa wakati wa ishara iliotabiriwa na Samueli mlamani kuonekana. Watu waovu walifanya mzaha na kuuliza; iko wapi hiyo ishara ya kuja kwa mwokozi wao? Wakati umepita kama vile ilivyo zungumzwa na manabii.

Wasioamini walitoa agizo; kama ishara iliyotabiriwa na Samuel mlamani haitaonekana kwa siku tumeteua, wote ambao wanaamini katika unabii wa mwokozi watauliwa.

Nefi alienda mpaka nyikani kuomba mwenyewe kwa niaba ya watu na kuombea ishara ikuje ili watu kusudi wasamehewe. Ndipo Mungu akanena kwa Nefi, usiogope Nefi, kesho ishara iliotabiriwa na nabii itakuja.

Siku ya pili wale wote ambaye waliamini maneno ya Nabii na walio tazamia kwa ishara iliotabiriwa na Samueli; mlamani walishikwa. Viongozi waovu wa Zarahemia walikuwa wanaenda kuwaua wakati jua linaenda kushuka kama ishara ya siku na usiku na siku bila giza haitakuja. Wote walingoja, wakatazama mbingu. Jua lilishuka lakini hakukuwa na giza. Ilimulika yenye kungaa zaidi katika mbingu nyota ambaye yeyote hajawai kuona. Ishara iliotabiliwa na Samueli mlamani ilikuja na wote walifahamu yakwamba Yesu kristo, mwana wa Mungu, amekuja ulimwenguni.

### *Giza Na Uharibifu*

Upesi gani watu walivyo msahau Mungu mara nyingine. WaNefi wakawa na majivuno tena; kujisifu zaidi kuliko walivyo kuwa hapo mwanzo. Nchi nzima ilitawanyika kuwa watu vikundi, matajiri na maskini. Hata kanisa ilitawanywa. Ni matajiri pekee waliweza kuenda shuleni na waliwadharau maskini kwa sababu hawakusoma. Ingawa matajiri waliongea maneno maovu kwa watu maskini, maskini wanyenyekevu ambaye walimwamini Mungu hawakuwajibu na maneno ya ukali; afadhali walimtumainia Mungu kuwapa faraja.

Muamuzi mkuu wa nchi aliuliwa na serikali ilianguka, ambaye ilifanya watu kutawanyika kuingia makabila. Vile shetani alivyo endelea kuvuruga mioyo za watu kutenda maovu, Mungu alituma manabii katika nchi kuwaonya watu wabadilike. Walakini, ni wachache pekee waliamini maneno ya manabii, na waovu waliwaaua badhi ya manabii. Ilikuwa sasa miaka therathini na tatu tangu Yesu alipozaliwa. Waumini walianza kuangalia kwa ishara ya kifo chake. Miaka therathini na nne [34] kutoka mwokozi azaliwe, ishara ya pili ikaja. Wingu likawa nyeusi na mvua ilimiminika chini na radi ilitikisa ardhi. Mwangaza ulipiga kwa nguvu Fulani ambaye mji wote ulichomeka. Nchi ilianza kupasuka kando kwa tetemeko la ajabu na miji mingine ilifunikwa na mchanga huku mingine ikianguka baharini. Kwa masaa matatu nguvu za Mungu zilitikisa nchi.

Katika nchi nzima kulisikika sauti ya kilio na maombolezo. Giza kamili ilitua juu ya nchi kama moshi. Jua, mwezi na nyota zilikataa kuangaza. Katika giza nzito hakuna hata mshumaa ungewaka. Hakuna moto ungewasha na hakukua na mwangaza ulioneka na kwa sababu ya ukuu wa umande wa giza ambaye ulikuwa mweusi pekee kwa siku tatu.

Kutoka gizani kulitoka sauti nemewaokoa kwa sababu mlikuwa wenye haki saidi kuliko ndugu zenu, ambao waliwaua manabii na mlisikiza watumishi wangu. Mimi ni kristo Yesu; niliumba mbingu na nchi. Mimi ndiye nuru ya ulimwengu.

## <u>KUTOKEA KWA YESU KRISTO</u>

### *Maneno Ya Manabii Yatimilike*

(3Nefi 4: 61-64; 3Nefi 5:1-17)

Katika siku ya nne upepo uliendelea kuwa tulivu na nchi iliacha kutikisa. Giza kilinyanyuliwa na watu walikusanyika ndani ya Hekalu katika sehemu inayoitwa nchi ya wingi. Walivyoangalia pande zote katika nchi yao walishangaa. Mahali ambaye kulikuwa laini ilirundikana pamoja na kusanyiko la miamba. Ujenzi uliwekwa kwa maangamizi; sehemu nyingine za nchi ilikuwa imegawanyika kwenda chini mahali papitapo mto na milima ilifunika mahali palikuwa miji mikuu ilikuwa imesimama hapo kale.

Ndipo sauti ilisikika kutoka mbinguni. Haikukuwa yenye sauti kuu, walakini iligusa mioyo yao kwa nguvu kuu. Waliangalia kuelekea mbingu na walisikia maneno tena; Tazama mwanangu mpendwa, msikilize. Akishuka kutoka mawinguni alikuwa mtu aliyevaa katika nguo nyeupe. Yesu kristo alishuka na kusimama mbele ya umati na alinyosha mikono yake. Ndipo akasema; Tazama mimi ni Yesu Kristo ambaye manabii wameshuhudia atakuja ulimwenguni.

Watu walianguka kwa magoti yao mbele ya Yesu na aliwambia; njooni na mguse alama ya misumari katika mikono yangu ili muweze kujua yakwamba niliuliwa kwa dhambi za watu wangu. Moja kwa moja umati uliendа mbele. Wote mara moja walilia, Hosanna, Libarikiwe jina la Mungu aliye juu zaidi.

## *Yesu Aliita Wanafuzi*

(3Nefi 5:18-22, 45-115; 3Nefi 6:1-37; 3Nefi 8:1-41)

Wakati umati ulipotulia, Yesu aliita Nefi kuja mbele. Nefi alikuja na kuanguka kifudi fudi kwa miguu ya



Bwana. Yesu alimwambia Nefi ya kwamba atampa uwezo wa kubatiza watu hawa na hapo Yesu aliwaita wanaume wengine kumi na moja na pia aliwapa uwezo wa kubatiza. Tazama mtaenda chini na kusimama majini na katika jina langu mtawabatiza. Nitawambia vile matabatiza ili kusiwe na mabishano zaidi miongoni mwa watu.

Na sasa haya ndiyo maneno ambayo mtasema, mkiwaita kwa jina, mkisema; kwa uwezo niliopewa na Yesu kristo, Ninakubatiza kwa jina la baba, na la mwana na la Roho mtakatifu. Amen, Na hapo mtawatumbukiza katika maji na kuwatoa tena nje ya maji.

Tena Yesu alinyoosha mikono yake mbele kwa umati. Heri nyinyi ikiwa mtasikiliza maneno ya hawa kumi na mawili ambao nimewachagua kuwafundisha na kuwahudumia. Ndipo Yesu alifundisha umati kupendana, wenye upole na kusamaheana.

Mmtumaini Mungu kama mototo mdogo anavyo tumaini baba yake, tubu dhambi zenu, nyenyekea na kubatizwa.

Yesu aliwafundisha jinsi ya kuomba; wakati mnapoomba msifanye kurudia maneno sawa ama kuomba kama vile wanafiki, wakisimama katika masinagogi ama kwenye barabara ili wonekane na watu kwa kuwa wako na thawabu yao, walakini muombe kutoka rohoni mwenu.

Ndipo Yesu alizungumza tena kwa wanafunzi wake, nyinyi ndio nimechagua kuhudumia hawa watu. Msisumbukie maisha yenu ni nini mtakula, au ni nini mtakunywa, wala mtavaa nini. Je, si maisha yako zaidi ya chakula ama mavazi? Lakini tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake na hivi vitu vyote

vitaongezwa kwenu. Sasa nendeni na kufundisha hawa watu. Baada ya kwenda kwangu andika chini maneno yangu ili kwamba wengi waweze kuyasoma katika miaka ijayo.

Akiona watu walikuwa wamechoka, Yesu aliwambia; nendeni nyumbani kwenu, mpumzike na mfikirie vitu ambavyo mmevisikia. Njooni kesho na nitawafundisha mengi. Kama vile Yesu alielekeza macho yake tena kwa watu waliokusanyika mbele yake, na akaona kuwa wanalia na walikuwa wanamwangalia kwa uthabiti kama wanaotaka kumwomba akae nao kwa muda mrefu zaidi. Yesu aliweza kuona ya kwamba wengine wao walikuwa wagonjwa, viwete, viziwi na vipofu. Yesu alijawa kwa huruma kwenda kwa watu na ali.wambia kuwaleta wagonjwa kwake. Walisonga mbele na mmoja kwa mmoja, Yesu aliweka mkono wake juu ya kila mmoja wao na wote waliponywa.

Ndipo Yesu aliwambia kuwaleta watoto wao wote kwake. Aliwachukua watoto wadogo, mmoja mmoja, na kuwaombea baba kwa ajili yao. Ndipo Yesu alisema; tazama wadogo wenu, watu walipotazama kuona mbingu, zikafunguka na malaika wakiteremka kutoka mbinguni walishuka chini na walizunguka watoto pamoja na moto na kuwahudumia.

Yesu aliamuru wanafunzi kumi na mbili aliowachagua kuleta mkate na divai. Wakati walipoleta, aliumega mkate na kuutakasa na kila mtu alikula, ndipo wote walikunywa kikombe cha divai. Baada ya hawa kumi na wawili kushiriki katika mkate na divai, walipeana mpaka kwa watu waliokusanyika mbele yake. Wakati watu walipomaliza kula; aliwaambia wanafunzi wake; kutakuwa na mmoja atakayetawazwa miongoni mwenu na kwake nitampa uwezo kupeana kwa watu wa kanisa langu ambao watatubu na kubatizwa. Aliwamuru kufanya hivyo kwa ukumbusho wa mwili wake ambao aliwaonyesha.

Yesu aliwafundisha; inueni juu nuru yenu kwamba ili ingare juu ya ulimwengu. Tazama mimi ni nuru; nimetoa mfano mbele yenu. Aligusa kila moja wa wanafunzi wake na kuwabariki na wakati Yesu alipowagusa wote kulitokea wingu ambalo lilifunika umati na hawangemwona Yesu. Wakati walipokuwa wamefunikwa Yesu aliondoka kutoka kwao.

### *Yesu Akitimiza Huduma Yake Juu Ya Nchi*

(3Nefi 9: 1-43; 3Nefi 10: 27-32; 3Nefi 12: 8-22, 3Nefi 13: 28-41, 50-51)

Sasa Yesu alikuwa amepaa mbinguni na watu walirejea nyumbani kwao. Lakini uvumi uliendа nje yakwamba Yesu atarudi na kujidhihirisha mwenyewe tena kwa watu kesho yake. Watu wengi walifanya kazi usiku kucha kutimiliza kazi yao ili waweze kuwa huru kuenda kuona Yesu wakati atakapojidhihirisha tena.

Wakati kulikucha, wanafunzi wa Yesu walierekeza macho yao kwa umati uliokusanyika pamoja. Umati ulikuwa mkuu sana kwamba walisababisha kuwagawanya kwenye vikundi kumi na mbili tofauti ili kila mwanafunzi aweze kuwafundisha. Wanafunzi waliwafunza kupiga magoti na kuomba Mungu katika jina la Yesu na kufundisha maneno yale Yesu alikuwa amezugumza, bila tofauti yeyote kutoka kwa yale ambayo Yesu alizugumza.

Baada ya kuomba; Nefi alikwenda chini ndani ya maji na alibatizwa. Wakati alipotoka kutoka kwa maji alibatiza wengine kumi na wawili ambao Yesu alikuwa amewachagua kama wanafunzi wake. Walivyo

kuwa wakitoka ndani ya maji, walijazwa na roho mtakatifu na pamoja na moto na walizingirwa na moto ambao ulishuka chini kutoka mbinguni na malaika walikuja chini kutoka mbinguni na kuwahudumia. Na ikawa kwamba malaika walipokuwa wanawahudumia wanafunzi, Yesu alionekana katikati miongoni mwao. Yesu aliomba pamoja na watu wake, na aliomba kwa baba kwa wale ambao aliokuwa amewachagua. Yesu alienda mbali kutoka kwa umati na kujiinamisha mwenyewe ardhini na aliomba tena kwa baba, akisema Baba, ninakushukuru kwamba umewatakasa hawa ambao nimewachagua kwa sababu ya imani yao. Na ninawaombea wao, na wale pia wataamini kwa maneno yao. Siombei ulimwengu, bali hao ulionipa kutoka ulimwenguni, kwa sababu ya imani yao, ili waweze kutakaswa ndani yangu ya kwamba niweze kuwa ndani yao kama vile wewe, baba ulivyo ndani yangu, ili tuwe moja ili kwamba nitukuzwe ndani yao.

Na wakati Yesu alipokuwa amezungumza haya maneno, alikuja tena kwa wanafunzi wake, na aliwapata walikuwa wanaomba bila kuzidisha kwake. Na Yesu tena alienda mbali kidogo na kuomba kwa Baba katika lugha ambaye haiwezi kuzungumzwa ama kwandikwa na mwanadamu, lakini umati ulisikia yeye akiomba na mioyo yao ilifunguka, na waliweza kusikia ndani ya mioyo yao maneno ambayo aliomba. Wakati Yesu alipomaliza kuomba alirudi tena kwa wanafunzi, na alisema; sijaona imani kubwa kama hii miongoni mwa wayahudi wote.

Sasa hakukuweko na mkate wala divai iliyoletwa na wanafunzi wala na umati; walakini Yesu aliwapa mkate wanfunzi wale. Na wakati walipokuwa wamekunywa aliwamuru kwamba wamege mkate, na kuwapatia umati. Na wakati walipowapatia umati aliwapa pia divai kunywa, na kuwaamuru wapatie umati divai.

Ndipo Yesu alisema; yule ambaye anaula huu mkate; anakula mwili wangu kwa nafsi yake, na yule ainywaye hii divai anakunywa damu yangu kwa nafsi yake, na nafsi yake haitaona njaa wala kiu, lakini atajazwa.

Wakati umati walivyokula wote na kunywa, tazama, walijazwa na Roho, na walipiga kelele kwa sauti moja na kumtukuza Yesu ambaye wote walimwona na kumsikiza.

Hapo Yesu alianza kuwafundisha tena. Aliwafundisha matajili kuwalipa watumishi mishahara mizuri. Alifundisha watu wake kuangalia maskini, wajane na yatima. Aliwafundisha kupeana fungo la kumi, sehemu ya kumi ya kila walichonacho kwa Bwana. Aliwaahidi ya kwamba kama watafanya haya, watabarikiwa zaidi. Aliwamuru watu wake wasome maandiko ili waweze kuelewa maneno yake. Tena yesu aliita wagonjwa kwake kuponywa. Ndipo alipaa juu tena kwa babake mbinguni mara ya pili.

Kutoka wakati huo kuendelea, wanafunzi walianza kufundisha na kubatiza. Mungu alidhihilisha ishara na miujiza kwa wale ambao walitubu na walibatizwa. Wanafunzi walipokuwa wamekusanyika pamoja kufunga na kuomba, Yesu Kristo alitokea mara ya tatu. Aliwauliza ni nini watapenda kujua kuhusu mafundisho yake. Wanafunzi walijibu; tunataka kujua jina ambalo tutaita hili kanisa. Watu wanagombana jinsi ambalo wataita kanisa.

Yesu aliwambia; hawajasoma maandishi, ambayo yanasema lazima mjivike juu yenu jina la Kristo, ambalo ni jina langu? Kwani; kwa jina hili ndilo mtaitwa nalo katika siku ya mwisho. Na yeyote atakayechukua jina langu na kuvumilia hadi mwisho, huyo ndiye atakayeokolewa katika siku ya mwisho.

Chochote mtakachofanya, mfanye katika jina langu; kwa hivyo mtaliita kanisa kwa jina langu na mtamwita baba katika jina langu ili aweze kubariki kanisa kwa ajili yangu. Na linawezaje kuwa kanisa langu isipokuwa liitwe kwa jina langu. Kwani kanisa likiitwa kwa jina la Musa, hapo litakuwa kanisa la Musa; au likiitwa kwa jina la mtu, hapo litakuwa kanisa la Mtu; lakini likiitwa katika jina langu, kanisa la Kristo, hapo basi litakuwa kanisa langu; ikiwa kwamba watajengwa juu ya injili yangu. Na ikiwa kanisa limejengwa juu ya injili yangu hapo Bwana ataonyesha kazi yake ndani yake.

### ***Wanafunzi Watatu Wenye Lami Juu Ya Nchi***

(3Nefi 13:12-34)

Hapo yesu alipokuwa amemaliza kufundisha; aliwazungumzia wanafunzi wake kila mmoja na aliwauliza; ni kitu gani ambacho mnahitaji kutoka kwangu baada yangu kwenda kwa baba?

Wote walisema, isipokuwa watatu, wakisema; tunataka kwamba baada ya kuishi maisha yetu, kwamba huduma yetu ambayo umetuitia iweze kuisha, na kwamba tuje kwako, kwenye ufalme wako. Yesu aliwambia; heri kwenu, kwa sababu mnataka kitu hiki kutoka kwangu; kwa hivyo baada ya kuhitimu miaka sabini na miwili, mtakuja kwangu katika ufalme wangu; na pamoja nami mtapata mapumziko.

Ndipo Yesu alisungumza kwa wale watatu ambao hakukuwa amewazungumzia na akawambia; ni kitu gani ambacho mnataka niwafanyie nitakapokwenda kwa Baba? Waliogopa kuzungumza kile ambacho wanataka kutoka kwa Yesu. Ndipo Yesu aliwambia; ninajua mawazo yenu, ya kwamba mnataka kitu ambacho Yohana, mpendwa wangu, ambaye alikuwa na mimi katika Yerusalem, alitaka. Kwa hivyo heri zaidi kwenu kwani hamtakufa, lakini mtaishi, kuona matendo yote ya Baba, mpaka nitakapokuja katika utukufu wangu, pamoja na uwezo wa mbinguni; na hamtapata maumivu ya kifo; lakini wakati nitakapokuja katika utukufu wangu, mtabadilishwa katika kufumba na kufumbua macho, kutoka hali ya kufa hadi kwa hali ya kutokufa; na ndiposa mtabarikiwa katika ufalme wa Baba yangu. Na haya yote nitafanya ili muweze kuleta mioyo mingi ya watu kwangu, wakati ulimwengu utakaposimama.

Ilikuwa wakati wa Yesu kurudi kwa Baba yake mbinguni. Aligusa kila mmoja wa wanafunzi wake, wote isipokuwa wale watatu ambao wataishi milele. Mbingu zilifunguka na Yesu alichukuliwa na wale wanaume watatu hewani. Waliguezwa kwa ghafula na kutoka wakati huo kuendelea hawatakufa kamwe. Ndipo wale wanafunzi watatu walibaki nyuma ulimwenguni na Yesu alikuwa ameenda.

### **Furaha Kuu Juu Ya Inchi**

(4Nefi 1-21)

Wanafunzi wote walienda nchini kote kote kufundisha injili ya Kristo na walianzisha kanisa la Kristo. Katika mwaka wa thelathini na sita baada ya kuzaliwa kwa Kristo, watu wote nchini wakiwa wanefi na walamani walimgeukia Bwana. Wanafunzi wa Yesu walifanya miujiza mikuu, kuponya wagonjwa, walifanya viziwi kusikia, vipofu kuona, vilema kutembea na hata walifufua wengine kutoka kwa wafu.

Bwana alibariki watu wake na walijenga miji mingi tena ambako iliohalibiwa katika wakati Yesu alisulubiwa. Kanisa ilikuwa na nguvu kwa sababu walikuwa wangalifu kwa kufunga na kuomba na kwa

kukutana pamoja siku zote kuomba na kusikia neno la Mungu.  Mioyo yao ilijawa na upendo wa Mungu na hakukuwa na mabishano miongoni mwa watu.  Hawakukua tena WaNefi au Walamani, matajiri au maskini.  Hawakukua wezi au wauaji nchini.  Upendo wao ulikuwa mwingi zaidi kwamba hakuna mmoja alikuwa na wivu au chuki kwa mwingine.

Wanafunzi wa kwanza walikufa na wengine wengi waliitwa na Mungu kujaza nafsi yao.  Hata hivyo watu waliishi na nguvu na uaminifu.  Ilikuwa sasa miaka mia moja na kumi tangu kuzaliwa kwa Kristo na wote ambao walikuwa wamemwona kristo walikuwa wamekufa, lakini watoto wao waliendelea kufundisha maneno ya Kristo na kwa kweli hakujakuwa na watu ambao wangekuwa na furaha zaidi.

# *MLANGO WA SABA*

# KUANGUKA KWA NEFI (DHAMBI YA WANEFI)

## <u>**MAANDIKO MATAKATIFU**</u>

### ***Ammoroni Akiyazika Maandiko***

(4Nefi 22:59)

Katika MWAKA huu wa mia mbili na moja kulianza kuwa miongoni mwao wale ambao waliinuliwa katika kiburi, kwa kuvaa nguo za thamani, na kila aina ya lulu nzuri, na vitu vizuri vya dunia.  Na watu walianza kujigawanya kwenye vyeo, matajiri na maskini.  Matajiri wakaanza kujenga makanisa yao kwa kujipatia faida, na waakanza kukataa kanisa la kweli la Kristo.

Na ikawa kwamba wakati miaka mia mbili na kumi ilipokuwa imepita kulikuwa na makanisa mengi katika nchi, ambayo yalidai kumjua Kristo, lakini walikataa sehemu kubwa ya injili yake.  Haya makanisa yalikubali aina yote ya uovu na kuongezeka sana kwa sababu ya uovu, na kwa sababu ya nguvu ya shetani ambaye alishikilia mioyo yao.

Wanafunzi watatu wa WaNefi ambao walikuwa wanaishi walihubiri kinyume na hii kanisa ya uovu.  Walitupwa gerezani lakini magereza hayakuweza kuwashikilia.  Magereza yalipasuka katikati na kuanguka chini.  Waliwatupa kwenye moto wa tanuu lakini wakatoka nje bila majeraha.  Na waliwatupa pia kwenye pango za wanyama wa mwitu, lakini walicheza na wale wanyama.

Ijapokuwa hiyo miujiza yote wasiomini walianza kuwapiga waumini hata zaidi.  Waumini walijiita waNefi na wasioamini waliitwa Walamani.  Walamani waliwafundisha watoto wao kuwachukia WaNefi.  Watu wakaendelea kuwa waovu, mpaka wasioamini wakawa wengi zaidi kuliko walioamini.

Nefi, mwanafunzi wakwanza aliyeitwa na Kristo alikuwa amechukua kazi ya kulinda maandiko matakatifu.  Alipeana hiyo kazi kwa kijana wake, Amosi.  Baada ya Amosi kufariki, kijana wake Amaroni akawa anaficha maandiko.  Baada ya miaka mia tatu na ishirini kupita, watu walibaki bado kwenye uovu

zaidi hata kwamba Roho wa Mungu alimwambia Ammoroni kuficha maandiko matakatifu ardhini ili kwamba yasihalibiwe.

### *Ammoroni Akimwagiza Mormoni*

(Mormoni 1:1-81; Mormoni 2:25-26; Mormoni 3:7-19; Mormoni 4:1-2)

Ijapokuwa huo uovu wote bado kulikuwa na watu wachache wazuri waliobaki katika nchi. Mmoja wa hawa watu wazuri alikuwa kijana aliyeitwa Mormoni. Wakati Mormoni alikuwa na miaka kumi pekee Ammoroni alimwambia; Mormoni, Naliona kwamba wewe ni mtoto mwenye bidii na ni mwepesi kwa kusoma. Ninataka wewe uangalie kwa uangalifu kila kitu ambacho kinatendeka pande zote zako. Wakati utakuwa karibu na umri wa miaka ishirini na nne, uende kwa nchi ya Antumu. Hapo nimeweka kwa ulinzi, katika kilima shimu, utapata maandiko matakatifu ya watu wetu. Ninataka uandike kwenye bamba vitu vyote ambavyo utakuwa umeviona kama vile ulikuwa unaendelea kukua. Mormoni aliahidi kufanya hivyo.

Kama vile miaka ilivyo pita, Mormoni alikumbuka ahadi zake kwa Ammoroni. Wakati Mormoni alikuwa na miaka kumi na moja, Walamani, na kwa miaka michache kulikuwa na amani katika nchi. Walakini, miaka michache kulikuwa ama kushukuru Mungu kwa ushindi wao. Watu wakawa waovu sana hata wanafunzi watatu wa WaNefi waliondoka katika nchi na Roho wa Mungu aliondoka kati yao. Hapakukua tena na uponyaji na miujiza.

Wakati Mormoni alikuwa na umri wa miaka kumi na mitano alitembelewa na Bwana na alikuja kutambua uzuri wa Mungu. Baada ya hii Mormoni alijaribu kuwahubiria watu . hawa lakini alikatazwa; watu walikuwa wa measi makusudi dhidi ya Mungu wao na maneno yaliyopeanwa na wanafunzi.

Na hawa wanyanganyi wa Gadiantoni, ambao walikuwa wameinuka tena juu wakati wa kwanza, walikuwa wameanza kunyanganya na kuua watu. Badala ya kutubu na kumuomba Mungu kwa usaidizi, watu walianza kuamini uganga na uchawi.

Mormoni alikuwa mkubwa kwa kimo, na mwenye nguvu na katika miaka kumi na sita ya ujana alichaguliwa kuongoza jeshi la WaNefi. Wakati Walamani walitushambulia tena kulikuwa vita kali mno na WaNefi wengi waliuliwa. Nchini kote kulisikika sauti ya kilio na maombolezo ya watu. WaNefi waliendelea kupigana hata ingawa walishindwa vita mara nyingi.

Wakati Mormoni alipofika umri wa miaka ishirini na nne, alikumbuka ahadi zake kwa Ammoroni na alienda mpaka kilima shimu na kuchimbua pamba takatifu. Aliandika juu ya hizo pamba hesabu kamili ya watu wake na uovu wao na machukizo, na hapo nikarudisha hizo kwenye ardhi.

Kwa sababu ya faraja ya Mormoni, WaNefi walishinda vita chache. Kwa miaka kumi walikuwa na amani katika nchi. Siku moja, bwana alimwambia Mormoni na kumuamuru awahubirie hawa watu. Mormoni aliwambia watubu na kujenga tena kanisa la uaminifu. Iwapo watafanya hiyo Mungu atawaokoa kutoka kwa adui zao, lakini hawakuweza kusikiliza.

Walamani walishambulia tena na WaNefi waliwashinda, lakini hawakushukuru Mungu kwa ajili ya ushindi wao; badala waliapa kwa kiti cha enzi cha Mungu kwamba hawataacha mpaka wawe wamelipiza

kisasi juu ya madui zao. Mormoni alihusunika sana kwa huu uovu mkuu kwamba alisema hatakuwa akiwaongoza kwenye vita.

Kwa miaka kumi na tano Mormoni .alisimama kando vile WaNefi na Walamani wakipigana. Miaka mia tatu na sabini na tano ilikuwa imepita tangu wakati wa Kristo. Mormoni aliweza kuona nchi nzima wanaenda kuanguka haraka kwa walamani. Alichimbua maandiko matakatifu kutoka kilima cha shimu na kuyachukua yote pamoja naye.

Moyo wa Mormoni ulijaa husuni kuona maangamizi makuu ya watu wake, WaNefi; yeye alikubali kuwaongoza mara nyingine. Vita iliendelea na kuendelea. Mormoni alikusanya watu wote pamoja katika nchi ya kumora. Hapo kumora kulikuwa vita kuu ya mwisho kati ya WaNefi na walamani. Wakati ilipoisha, ni watu ishirini na wane pekee wa WaNefi waliachwa hai. Vile Mormoni alivyoangalia kwa watu wote ambao walikuwa wameuliwa alilia na kusema; ilikuwaje mkamkataa Yesu, ambaye aliwangojea na mikono wazi kuwapokea?

Mormoni sasa alikuwa mzee kwa hivyo alimpa kazi ya kutunza maandiko matakatifu kwa kijana wake Moroni.

### *Moroni Akiandaa Maandiko Kwa Siku Za Mwisho*

(Mormoni 4:1-28)

Moroni aliandika wakati wa mwisho juu ya pamba kabla yao kufichwa katika kilima kumora. Aliandika kwa watu ambao wataweza kwa siku moja kusoma haya maandiko matakatifu. Ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwangu kumaliza haya maneno. Maneno ya watu ambao waliishi siku moja katika nchi hii watakuwa ushuhuda wa Kristo kwenu. Itakuwa kama wanaongea kwenu kutoka kwenye mavumbi.

Moroni aliachwa peke yake sasa, lakini alimtumainia Mungu na hakuweza kufa moyo. Vile Moroni alivyojificha kutoka kwa walamani, aliendelea kufupisha hesabu ilioandikwa juu ya pamba za dhahabu ishirini na nne zilizogunduliwa na watu wa Zarahemia katika nchi ya kaskasini, habari ya watu wanaoitwa kama Wayaredi.

# MLANGO WA NANE

# WAMULEKI

## KUHAMA KUTOKA YERUSALEMU

### *Kijana Wa Mfalme Zedekia*

(Omni 1:23-38; Helamani 3:56)

Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Zedekia, Bwana alikuwa ameagiza Lehi na jamii yake kuacha Yerusalemu. Sasa katika mwaka wa miatano na themanini na saba kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Mfalme Zedekia, mfalme wa Yuda alipelekwa mateka ndani ya Babeli.

Bwana aliamuru ya kwamba kijana mdogo wa Zedekia, bado alidhaniwa kuwa mtoto na watu waliobaki hai kwa familia ya Zedekia waondoke Yerusalem na hao pia walifika katika nchi mpya ngambo ya pili ya bahari na wanatajwa kama wamuleki. Mosia, mfalme wa WaNefi na mtoto wa Lehi, alikuwa ametoa kikundi cha wanaume kuenda nyikani, na walivumbua watu wa Muleki, ama Wamuleki, katika nchi ya Zarehemla. Waliwaita watu wa Zarehemla. Kwa wakati Mosia alifumbua hawa watu wa Zarahemia, walikuwa wameongezeka zaidi. Hata hivyo, walikuwa na vita nyingi na mapigano makubwa, na walikuwa wameangamia kwa upanga mara kwa mara lugha yao ilipata kubadili na WaNefi hawakuweza kuwasikia. Wamuleki hawakuwa wamebeba maandishi yoyote pamoja nao kuwakumbusha juu ya Mungu. Bila neno la Mungu walikana uwepo wa muumbaji.

Watu wa Zarahemia walifurahi sana kwa sababu Bwana alikuwa ametuma watu wa Mosia pamoja na bamba za shaba ambazo zilikuwa na maandishi ya Wayahudi. Mosia aliwafundisha lugha ya WaNefi na ikawa kwamba baada ya kufunzwa lugha ya Mosia, watu wa Zarahemia walitoa nasaba ya mababu zao, kulingana na ukumbuko wao. Na ikawa kwamba watu wa Zarehemla na watu wa Mosia waliungana pamoja na Mosia aliteuliwa kuwa mfalme wao. Wamuleki walikuwa pamoja nao jiwe kubwa lilokuwa na maandishi juu yake yalieleza historia ya mmoja aliyeitwa Koriantumuri, Myaredi wa mwisho na mauaji ya watu wake. Korinatumuri alivumbuliwa na watu wa Zarehemla; na aliishi nao kwa muda wa miezi tisa.

## *MLANGO WA TISA*

# NCHI YA YAREDI

***Watu Kutoka Mnara Wa Babeli***

(Etheri 1:7-27, 36-85; Etheri 3:1-14)

Historia ya Wayaredi ilianza na mtu mmoja aliyeitwa Yaredi ambaye alikuja kutoka mnara mkuu uliojengwa kufika mbinguni katika nchi ya shina. Huu ulikuwa wakati Bwana alipochanganya lugha za watu, na kuwatawanya juu ya uso wa dunia nzima.

Yaredi aliuliza kaka yake, ambaye alikuwa mtu mwenye nguvu na aliyependelewa sana na Bwana, kumsihi Bwana kwamba asichanganye lugha yao ili waweze kuendelea kuelewana wao kwa wao. Kaka wa Yaredi alimwomba Bwana na Bwana alikuwa na huruma juu ya Yaredi; kwa hivyo hakuchanganya lugha yao. Halafu Yaredi akamwambia kaka yake omba tena kwa Bwana na iwe kwamba asiwe na hasira kwa

wale ambao ni marafiki zetu, ili kwamba asiwachafulie lugha yao. Na ikawa kwamba kaka wa Yaredi aliomba Bwana na Bwana akawa na huruma kwa marafiki zao na jamaa zao pia.

Yaredi alimzungumzia kaka yake tena, akisema; nenda na ukamwulize Bwana kama atafukuza kutoka nchini na ikiwa atatufukuza kutoka nchini, muulize kule ambako tutaenda. Kaka wa Yaredi alimwomba Bwana ni wapi wanaweza kuenda, na Bwana alimjibu; nenda na ukakusanye pamoja wanyama wako, wote wa kiume na wa kike wa kila namna; na pia mbegu ya nchi ya kila namna, na jamaa yako; na pia Yaredi kaka yako na jamaa yake; na pia marafiki zako na jamaa zao; na marafiki wa Yaredi na jamaa zao. Mungu aliwaongoza njiani mpaka baharini. Wakati walipofika kwenye bahari, kila mmoja alikuwa amechoka kutokana na safari yao ndefu. Walipiga hema na wakaishi katika hema kwenye ukingo wa bahari kwa muda wa miaka miine.

Vile walivyo ishi kwenye ukingo wa bahari, bwana aliwamuru kufanya kazi na kujenga mashua nane kuwapeleka juu ya bahari mpaka kwenye nchi mpya. Haya mashua yalijengwa kwa namna ya mafunzo ya Bwana. Yalikuwa madogo na yalikuwa mepesi juu ya maji na yalijengwa kwa aina moja kwamba yalikuwa yamekazwa sana na yangeshikilia maji kama vile sahani inavyofanya. Kulikuwa na tundu upande wa juu na pia upande wa chini; wakati mtakapokosa hewa mtafungua tundu na mpokee hewa. Na ikiwa itakuwa kwamba maji yataingia ndani kwenu tazama mtafunga tundu ili msife maji na kuangamia.

Mungu akasema; ninaenda kutuma upepo mkali kuwasuguma juu ya bahari. Wakati mwingine upepo utafanya mawimbi kuwa kubwa kama milima na kusukuma mashua chini ya mji.

Wakati mashua yaliyoisha walishangaa kama bwana atakubali wavuke haya maji mengi kwenye giza. Kaka wa Yaredi alijua Mungu anaweza kuweka mwangaza katika mashua kwa hivyo alipanda mlima na kuchukua kutoka kwa mwamba mawe madogo kumi na sita. Haya mawe yalikuwa meupe na safi hata kama kioo kilicho wazi. Kaka wa Yaredi ndipo aliyabeba katika mikono yake hadi juu ya kilele cha mlima, na akaomba tena kwa Bwana, akisema; Ee Bwana, umesema kwamba lazima tuzungukwe na mafuriko. Ee Bwana; usikubali kwamba wavuke hii bahari katika giza, lakini tazama haya mawe ambayo nimechonga kutoka kwa mlima. Ninajua, una uwezo wote, na unaweza kufanya chochote upendacho kwa faida ya binadamu; kwa hivyo gusa haya mawe na kidole chako, na utayarishe kwamba yaangaze kwenye giza, ili tuweze kuwa na mwangaza tutakapovuka bahari.

Na pazia ilitolewa machoni mwa kaka wa Yaredi na aliona kidole cha Bwana kiligusa yale mawe moja moja. Kaka wa Yaredi alishuka chini kutoka kwenye mlima, na kuweka mawe mawili moja kwa kila mashua.

Yaredi na wale waliokuwa pamoja walitupwa juu ya mawimbi ya bahari na mashua ilisukumwa na upepo na mawimbi kwa siku mia tatu arubaini na nne kabla ya kufika kwenye nchi ya hadi.

Watu waliokuja pamoja na Yaredi, walioitwa wayaredi, walijua hii nchi ya hadi ilikuja pamoja na masharti; kwa kuwa Bwana alisema; na sasa tunaweza kuona agizo la Mungu kuhusu hii nchi, ya kwamba ni nchi ya hadi, na taifa lolote itakayemiliki nchi hii, lazima wamtumikie yule Mungu wa kweli, au waangamizwe uujalivu wa ghadhabu yake ukiwajia. Na ujalibu wa ghadhabu yake huja juu yao baada ya wao kuwa waovu sana; kwani tazama, hii ni nchi ambayo ni nzuri kuliko nchi zingine zote; kwa hivyo yule

atakayemiliki atamtumikia Mungu; au wataangamizwa; kwani ni amri ya milele ya Mungu. Na haitakuwako mpaka ujalivu wa uovu miongoni mwa watu wa nchi hii, ndipo wataangamizwa.

Wakati watu waliweka miguu yao juu ya ukingo wan chi ya ahadi walisujudu na kumshukuru Mungu kwa baraka zake.

***Mfalme Wa Watu Wa Yaredi***

**(**Etheri 3:15-48; Etheri 4:1-7)

Mungu alibariki watu wa Yaredi walivyoishi katika nchi mpya. Kaka wa Yaredi alikuwa kiongozi wa kiroho wao na aliwafundisha kumfuata Mungu kwa unyenyekevu. Wakati Yaredi na kaka yake walipata kuwa wazee walitaka kubariki watu wao kabla hawajaenda nyumbani kwa Bwana. Walikusanya watu pamoja na kaka wa Yaredi aliuliza watu; ni kitu gani mtakachohitaji kutoka kwetu kabla hatujaenda kwenye makaburi yetu?

Watu walitamani ya kwamba waweze kuchagua mfalme atakayewaongoza. Kaka wa Yaredi aliwaonya; kweli kitu hiki kitawaongoza kwenye utumwa. Lakini watu walisisitiza juu ya mfalme kuwa kiongozi wao.

Yaredi alisema kwa kaka yake awakubalie watu wawe na mfalme wao, na walimchagua Pagagi, mwana wa kwanza wa kaka ya Yaredi. Pagagi, hata hivyo alikataa kuwa mfalme wao vile walivyofanya vijana wengine wote wa kaka wa Yaredi. Wana wa Yaredi nao pia walikataa kuwa mfalme, isipokuwa tu mmoja, jina lake aliitwa Oriha, na alitawazwa kuwa mfalme juu ya watu wa Yaredi.

Yaredi na kaka yake walifariki na kaka yake na Oriha akawa mfalme. Oriha alijinyenyekea mbele ya Bwana na aliongoza kwa haki, na badala yake mwana wake Kibu alitawala pia kwa haki.

Kibu alikuwa na kijana aliyeitwa Korihori ambaye alikuwa muasi dhidi ya baba yake na alichukua watu wengi mbali kuishi katika nchi inayoitwa Nehori. Huko alikusanya pamoja jeshi na alikuja kwenye nchi ya ufalme wa Baba yake na kumchukua mateka, ambako kulileta kutimia msemo wa kaka ya Yaredi kwamba watawekwa kwenye utumwa.

Wakati ule Kibu alikuwa akiishi utumwani alipata kuwa mzee sana; walakini Kibu alimzaa Shule. Wakati Shule alikuwa mkuu kwa miaka alipata kuongezeka nguvu, na kuhukumu. Alimkasirikia kaka yake. Shule alienda kwenye kilima cha Efraimu, na alitengeneza mapanga kutoka kwa chuma kwa ajiri yake na wale ambao watamsaidia kuchukua tena ufalme.

Akijiamia kwa panga alirejea kwenye mji wa Nehori na kupigana vita na kaka yake Korihori. Shule alishinda na alijipatia ufalme na kurudisha kwa baba yake, kibu kwa sababu ya kitu ambacho Shule alifanya, baba yake alimpa ufalme na alitawala badala ya baba yake. Shule aliongoza kwa haki na ufalme wake uliongezeka katika hesabu na Shule pia alizaa wana na mabinti wengi.

Wakati Shule alikuwa mzee alipeana ufalme kwa mwana wake Omineri ambaye pia alikuwa mfalme aliemcha Mungu. Omineri alikuwa na kijana aliyeitwa Yaredi ambaye alitamani ufalme kwake mwenyewe. Yaredi alichukua nusu ya ufalme wa baba yake na akamweka baba yake kwenye utumwa. Wakati alipokuwa katika utumwa Omineri alikuwa na vijana wengi ambao walikomaa na kushinda kaka yao Yaredi.

Yaredi aliwasihi kwamba wasimuue na kaka zake walimwachia maisha yake na kumuacha hai. Yaredi hakuweza kuridhika pamoja na msamaha alionyeshwa na kaka zake; matumaini yake yalikuwa kurudisha na kupata tena ufalme. Yaredi alikuwa na binti ambaye alikuwa mrembo sana lakini moyo wake ulikuwa muovu kama ule wa baba yake. Binti wa Yaredi alimwambia mpango wake vile ataweza kusaidia baba yake kurudisha ufalme. Alimwambia baba yake; alika rafiki yako, Akishi kwa chakula. Mimi ni mrembo sana. Nitacheza mbele yake na atatamani kwamba niwe mke wake. Umwambie kwamba hatanioa mimi isipokuwa akuletee kichwa cha baba yako, mfalme.

Yaredi alimwalika Akishi kwa chakula na kila kitu kikafanyika vile walivyopanga na Akishi alikubali kumuua mfalme Omineri ili aweze kumuoa binti wa Yaredi.

Mungu alimwonya Omineri kwenye ndoto kwamba aondoke nje ya nchi. Omineri na jamaa yake waliokoka lakini Yaredi alitawazwa juu ya ufalme. Akishi hakuridhika kupata mke mrembo; alitaka kuwa mfalme pia. Pamoja na usaidizi kutoka wale ambao alikuwa amewaapisha kwa kiapo alimuua Yaredi, na alipata kuwa mfalme.

### *Maangamizi Ya Taifa Ya Yaredi*

(Etheri 4:32- Etheri 6:109)

Zaidi ya miaka mingi, Wayaredi walijenga miji mingi mikuu na watu wao walihifadhi sehemu nyingi ya nchi. Wakati wafalme wanaomwogopa Mungu waliyetawala, watu waliweza kubarikiwa, lakini wakati wafalme waovu waliotawala, nchi ililaaniwa.

Mfalme mmoja muovu aliyeitwa Hethi alimuua Baba yake mwenyewe na kuchukua utawala wake. Wakati wa Hethi Mungu alituma manabii popote nchini wakiubiri onyo la Mungu kwa watu; lazima mtubu kama sivyo kungekuwa na njaa kuu katika nchi.'

Watu wa Yaredi hawakuamini na waliua wegine wa manabii na walitupa wengine nje ya nchi. Ndipo mvua ilisimama na mazao yao yalikauka katika mashamba. Lakini hii siyo laana yote iliyokuja juu yao. Mungu aliamuru nyoka nyingi ya sumu kutokea juu ya uso wa nchi. Kondoo, mbuzi na ngombe waliogofya walikimbia kutoka kwa nyoka na upesi hakuna kitu kilibaki kukuliwa. Katika taabu yao, watu walitubu na walirudi kwa Mungu. Wakati Mungu alipoona walikuwa wamenyenyekea kwa ukweli, alituma mvua kurudi katika nchi na kuondoa mbali nyoka wa sumu, kwa wakati watu walishi katika uadilifu wakiongozwa na mfalme mcha Mungu aliyeitwa Libu. Hakuna watu waliobarikiwa kulilko wao. Walakini wafalme wengi waovu walichukua utawala na watu wayaredi walirudi kwa njia zao mbaya.

Mwishoni, katika siku za utawala wa koriantumuri, Mungu alituma nabii mmoja mkuu wa mwisho aliyeitwa Etheri. Etheri alihubiri kutoka asubuhi hata kwenda chini kwa jua akihimiza watu kutubu au

wataweza kuangamizwa na nchi yao iweze kupeanwa kwa watu wengine.  Watu walikataa kusikia maneno ya nabii.

Mtu anayeitwa shizi alikuwa anajaribu kuchukua ufalme wa Koriantumuri ambao ulileta vita vya wenyewe kwa wenyewe kutokea katika nchi.  Bwana alimuamuru Etheri kuenda na kutoa unabii kwenda kwa koriantumuri, ya kwamba kama anaweza kutubu, na nyumba yake yote nzima, bwana ataweza kumrudishia ufalme wake, na kuacha watu.  Kama Koriantumuri akikataa kutubu ndipo watu wake na nyumba yake yote inaweza kuangamizwa, na Etheri ataweza pekee kuishi kuona watu wengine kuchukua hii nchi ya ahadi.

Koriantumuri hakutubu; wala nyumba yake haikutubu wala watu.  Vita vya wao kwa wao viliendelea mbele na watu walitaka kumuua Etheri alitorokea na kujificha tena kwenye pango la ule mwamba.  Mchana na katika usiku aliondoka nje kuona maangamizi ya watu wake.



Baaba ya miaka minne vita vilikuwa vikubwa na vya kudumu kwamba uso wan chi ulifunikwa na miili ya waliokufa na hakukuwa na aliyebaki kuzika waliokufa.  Jeshi liliendelea mbele kutoka kwa umwagaji wa damu hadi kwa umwagaji wa damu mwingine, wakiacha miili ya wote wanaume, wanawake, na watoto imetawanyika juu ya uso wa nchi.

Majeshi sehemu mara mbili walikusanyika kwa hivyo vita yao vya mwisho. Kila siku walipigana siku nzima na kulala juu ya panga zao usiku huo.  Kila siku wengi waliuliwa na watu wachache walibaki kupigana.  Baada ya siku nyingi za vita, Shizi na Koriantumuri ndio pekee walibaki wakisimama.  Koriantumuri aliua Shinzi, na hapo alikumbuka unabiii wa Etheri; wewe utaachwa pekee yako.

Etheri alivyoangalia kwenye vita vilipopiganwa aliona wayeredi wote walikuwa wamekufa isipokuwa mtu mmoja, Koriantumuri.  Etheri alimaliza kwandika historia ya uharibifu wa watu wake, na hapo alimalizia maandiko yake pamoja na maneno yake mwenyewe; haidhuru kama bwana anataka kunichukua nikiwa hai au kama nitakufa.  Yote ambayo yananipasa ni kwamba nimeokolewa katika ufalme wa Mungu.  Koriantumuri aliendelea kuishi mpaka alivumbuliwa na watu wa Zarahemia.  Hapo alikufia kati ya watu wageni vile Etheri alivyotabiri.

# *MLANGO WA KUMI*

# MANENO KWA KIZAZI KIJACHO

## <u>MORONI AKITIA MUHURI MAANDIKO</u>

***Maagano Ya Mwisho***

(Moroni 10:3-5, 31)

Moroni alivyokuwa akitia muhuri maandiko aliandika ujumbe moja wa mwisho kwa watu ambao watakuwa wakisoma kitabu cha Mormon katika siku za mwisho.  Tazama, ningewashauri kwamba mtakaposoma vitu hivi, ikiwa, itakuwa hekima katika Mungu kwamba muyasome, kwamba mngekumbuka jinsi vile Bwana amekuwa na huruma kwa wanadamu, kutokea kuumbwa kwa Adamu, hadi chini mpaka wakati ambapo mtapokea vitu hivi, na kuitafakari katika mioyo yenu.  Na wakati mtakapopokea vitu hivi, ningewashauri kwamba mngemuuliza Mungu, baba wamilele, katika jina la Kristo, ikiwa vitu hivi si vya kweli; na ikiwa mtauliza na moyo wa kweli, na kusudi halisi, mkiwa na imani katika kristo, atawaonyesha ukweli wake kwenu, kwa uwezo wa Roho mtakatifu; na kwa uwezo wa Roho mtakatifu mtajua ukweli wa vitu vyote.

Moroni alimalizia ujumbe wake pamoja na maneno ya unyenyekevu; na sasa nawaaga kwenu nyote, kwaheri.  Heri karibu nitaenda kupumzika katika paradiso la Mungu, mpaka roho yangu na mwili itakapounganishwa tena, na niinuliwe juu kwa ushindi kupitia angani, kukutana na nyinyi mbele ya kiti cha enzi cha kupendeza cha yule yehova mkuu, mwamuzi wa milele wa wanaoishi na waliokufa.  Amina.

*MWISHO.*